Sudan Kusini

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 4

**Kiswahili kwa kidato cha Nne(4)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

Sudan Kusini

Kitabu cha mwanafunzi

Kiswahili 4

Kidato cha Nne



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

## Mambo muhimu ya kuzingatia.

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

## Mambo unayokatazwa kufanya.

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
4

# Kiswahili

*Kitabu cha Mwanafunzi*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION.
All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder. Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na ya Elimu na Mafunzo.

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

FOREWORD

I am delighted to present to you this textbook, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This textbook shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum and school textbooks for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum and the new textbooks. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my previous role as the Undersecretary of the Ministry, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)

**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO

MAAMUZI YA MAISHA NA MATATIZO ZA KIJAMII .............. 1
USAWA WA JINSIA .......................................................... 26
UHUSIANO WA KIMATAIFA ............................................... 41
UTALII......................................................................... 63
TAMADUNI, URITHI NA UTAMBULISHO ............................. 72
HAKI ZA MWANANCHI.................................................... 78

# SURA YA 1

# MAAMUZI YA MAISHA NA MATATIZO ZA KIJAMII

## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

**Soma shairi lifuatalo.**

### Hakiba hii mwafaka

Nipulikize neleze, yaloniswibu rohoni,
Kwa yakini ndo muweze, mfanikiwe jamani,
Darahimu msipoteze, myahifadhi nawambeni,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Hakiba hii mwafaka, hautapata dosari,
Takuauni hakika, mweledi pia mahiri,
Seni ondoa mashaka, kwa kweli takuwa heri,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Ujana kweli ni moshi, ujipange barabara,
Ndio upate kuishi, uepuke masihara,
Mithili na Yule mwashi, ajipatia mshahara,

Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Tuwe walio busara, tuweke ya baadaye,
Ndio tukuwe imara, tufue dafu keshoye,
Tutaacha ufukara, tafaulu baadaye,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Manju miye ninahoja, muyaweke mawazoni,
Hakiba sio vioja, ni bayana maishani,
Nataka muone haja, mpate hamu na imani,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Mswahili sitasita, kunga'mua ya moyoni,
Aila yako kupata, taadhima duniani,
Hautapata matata, Jalali takuauni,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

Yameisha maandiko, kaeleza ya hekima,
Hata ukipata jiko, utajapata heshima,
Ninawapa wao heko, walojikaza daima,
Malenga ninadokeza, hakiba hii mwafaka.

## Maswali

1. Mwandishi anasema tuhifadhi nini katika ubeti wa kwanza?
2. Taja muundo na umbo la shairi hili.
3. Ubeti wa nne unasema tutapata nini tukiekeza?

4. Taja dhamira ya mshairi.
5. Ni maudhui yepi yanayojitokeza katika shairi nzima?

**Shairi b**
**Soma shairi lifuatalo.**

**Usife moyo**

Malenga nang'amua, yalo yakini maana,
Kuwa na ari nakwambia, atakuwezesha Rabana,
Wengi takuchekelea, kukukejeli kweli sana,
Usife moyo mwandani, Rabuka ni muauni.

Mwanagenzi jizatiti, masomo ni ngao yako,
Utakuwa madhubuti, ufanisi huko kwako,
Usitegemee bahati,tafuta wewe vitu vyako,
Usife moyo mwandani, rabuka ni muauni.

We rijali sikasiri, vumilia kwa hasara,
Bilashaka tia ari, uepuke masihara,
We usiwe na kiburi, nyenyekea kila mara,
Usife moyo mwandani, rabuka ni muauni.

Subira huvuta heri, itafika siku njema,
Utapata utajiri, ufanisi ninasema,
Hutarudi huko misri, mambo yako kuwa mema,
Usife moyo mwandani, rabuka ni muauni.

Ulokwama kwa mapenzi, utafaulu hakika,
Utampata huyo mpenzi, ndo kisura bilashaka,
Mchumba atakuenzi, hautakuwa na shaka,
Usife moyo mwadani, rabuka ni muauni.

Na kilele nimefika, yameisha maandishi,

Ya hekima nimefoka, mfahamu dio muishi,
Msipate kuteseka, mfanikiwe kwa aushi,
Usife moyo mwandani, rabuka ni muauni.

## Maswali

1. Mwandishi anahimiza nini katika ubeti wa 1
2. Ubeti wa 2 unamlenga nani?
3. Ubeti wa nne unazungumzia nini?
4. Anayelengwa katika ubeti wa tano anakosa nini?
5. Taja dhamira ya mshairi.

## Shairi c

**Soma shairi lifuatalo.**
**Subira huvuta heri**

Miye hapa nang'amua, yalojaa mumoyoni,
Kishaye mtafurahia, yake Mola maishani,
Ndiye miye nelezea, ushikilie imani,
Subira huvuta heri, mwandani ninakweleza.

Yule asovumilia, atamlaumu rabuka,
Kwa shida alopitia, ya maishani hakika,
Bahari taogelea, ya taabu bilashaka,
Subira huvuta heri, mwandani ninakweleza.

Mwanagenzi wewe soma, utilie maanani,
Utavuna yalo mema, faida kwako usoni,
Ya hekima ninasema, ni bayana maishani,
Subira huvuta heri, mwandani ninakweleza.

Na unayependa Mola, mtumikie kulihali,
Utafaulu inshala, mkimbilie akujali,
Utapata nazo hela, Mungu takupa kibali,

Subira huvuta heri, mwandani ninakweleza.

Unotafuta ajira, umwamini Maulana,
We usiwe na marara, takuauni Rabana,
Wewe kuwa na subira, utaelewa maana,
Subira huvuta heri, mwandani ninakweleza.

*Imenukuliwa kutoka kwa* Mugun Wycliffe

**Mada Ndogo ya 2:** Kusoma

**Kifungu a**
**Soma kifungu kifuatacho.**

Maisha ya binadamu yamepitia katika hatua mbalimbali katika karne kadhaa zilizopita. Watu husema mengi kuhusu maisha. Wengine husema kuwa mtu anapozaliwa hatima yake huwa imeshaamuliwa na mwenyezi na hata afanye nini hakuna wa kuibadilisha. Yaani wanaamini kuwa, kama mtu amejaaliwa awe mwizi stadi maishani basi atakuwa mwizi stadi bila shaka; kama majaliwa yake ni awe daktari maarufu, basi atakuwa daktari maarufu na kadhalika.Lakini kulingana nami hatima ni hali ile mtu anajiamulia yeye mwenyewe.

Katika ulimwengu waleo kuna baadhi ya watu ambao bado wanaamini kuwa wanapozaliwa kazi yao kuu ni kuponda raha kwani hatima yao Mungu anaijua.Jambo hili limewaathiri vijana kwa kiwango kikubwa;asilimia kubwa ya vijana wanaishi katika ufukara kutokana na tabia hii.

Vijana ni lazima wajue maisha hutegemea mipango na juhudi. Mtu asipojibidiisha na kupanga maisha yake inavyofaa, basi bila shaka mambo

yatamwendea vibaya. Ukitazama vijana wengi, utaona kuwa hawana mwelekeo imara wa kuendesha maisha yao. Wao hushiriki chochote eti kwa kuwa tayari wamejaaliwa kesho yao. Wanapokuwa shuleni, wengi wao hawana haja na elimu. Wanaamini eti shuleni ni pahali pa kungojea utamu wa maisha. Wengine hujihusisha na vitendo vya ajabu kama vile kuchochea migomo, kutumia dawa za kulevya, starehe zisizo na mipango, kushiriki ngono kiholelaholela na mengineyo.Wengine ifikapo jioni hawapatikani tena shule kwani huwa wameyoyomea mijini na vitongojini kuponda raha.  Wengine ni majambazi sugu. Wao hushirikiana na wavunja sheria sugu kupora mali ya wenyewe bila mtu kuwashuku.

Wanafunzi wengine huifanya kazi yao kuu kuwa ile ya kuwahangaisha wenzao. Katika baadhi ya shule, wanafunzi hujihusisha na vitendo vya kuwadhulumu wenzao wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa kuwapiga, kuwafanyisha kazi ya sulubu hata vitendo vya ngono. Wengine wamefikia kiwango cha kuwatishana hata kuwapiga walimu wao. Hata wanapokuwa nyumbani huwa ni balaa tupu.

Mavazi yamekuwa jambo la kuzungumziwa kila uchao.Baadhi ya vijana huvaa mavazi ya ajabu. Wasichana huvaa nguo fupi utadhani wako uchi.  Pia baadhi ya wasichana wanavaa nguo zisizo na maadili nguo ambazo ni nyepesi zinazoonyesha nguo za ndani au vitopu na vimini vinavyoacha sehemu kubwa ya maungo yao nje wenyewe wanajiita “masista duu”.Wengine hutia herini chungu nzima masikioni na kujipaka rangi za kutisha mdomoni. Wengine hushrikiana kimapenzina wavulana na hata wazee ambao huwafurahisha daima kwa darahima kochokocho. Neno UKIMWI ni geni kwao.Si ajabu kuwa baadhi yao tayari wameenda jongomeo na wengine wako safarini kuelekea kuko huko. Isitoshe, wakikutana na kina dada watalii kutoka ng’ambo wanazuzuliwa na hizo ngozi zao nyeupe pepepe na kuapa kuwa iwe ni lazima watakuwa kama wao. Wanafanya juu chini kusaka ngwenje kokote zinakopatikana ili kujinunulia vipodozi aina aina vya kupaushia ngozi zao. Wasichana wengine hawasomi tena.

Wavulana nao hawaachwi nyuma.  Neno ‘nidhamu’ ni istilahi mpya kwao. Wao wanaishi leo, kesho ni majaaliwa. Baadhi ya vijana wa kiume imekuwa ni kawaida kuwa ametoboa masikio na kuvaa herini, wamesuka nywele na kupaka poda sura zao. Pia kuvaa suruali chini ya makalio yao.Wanavaa mikufu inayong’ara kuliko ile ya kina dada. Nayo mitindo ya nguo huzihangaisha akili

zao kutwa kucha. Macho na masikio yao hukaa chonjo kila dakika ili wafahamu ni mitindo ipi mipya iliyoingia hasa kutoka ng'ambo kunakoishi wazungu wenyewe. Wengine nywele wameziweka kalikiti. Suruali wanavaa zilizoganda mwilini utadhani zimepakwa gundi. Nao wengine wana mikururo ya marafiki wasichana. Ukiwauliza kisa na maana ya kutongoja hadi wakati ufike wanakwambia eti ndio mtindo.

Haya yote ni matokeo ya utandawazi na marafiki wamaya. Vijana wetu wanaiga mambo yasiyofaa kupitia mitandao ya kijamii iliyopo kila sehemu nchini.Ijapokuwa mitandao hii ina faida kama vile kuturahisishia mambo mengi yanayoendelea duniani na pia inawasaidia wanafunzi katika masomo yao lakini baadhi ya vijana wanaitumia vibaya kwa kuiga mambo yasiyofaa.Itafika wakati mzazi ataona aibu kumtambulisha mwanawe kwa rafiki zake kwa kukwepa aibu kutokana na mwanawe kutokuwa na maadili mazuri.

Hata hivyo, ni muhimu sana vijana kufungua macho yao ili kuona mwanga. Wanafaa kuelewa fika kuwa ujana ni moshi tu. Dakika hii upo, dakika nyingine ushatoweka. Ujana ni kipindi cha maisha cha kujifunga masombo kwa majukumu ya baadaye. Ni kipindi cha kujitafutia maarifa tunu. Iwapo hali ni kinyume, basi mambo hayana budi kwenda mrama.

Tusiwaache vijana wetu huru sana na huu utandawazi kwa sababu baadaye tutakuja kujuta watoto wetu watakapokuwa wameharibikiwa.Wazazi umefika wakati tuzungumze na vijana wetu ili tuweze kutayarisha viongozi wa baadaye.Viongozi mbalimbali wanajitahidi siku hadi siku kuzungumzia suala hili la maadili hasa tunapoona maadili yanadororakwa kasi tofauti na ilivyokuwa zamani kutokana na baadhi ya vijana kudharau na kutoziheshimu mila na desturi zao.Tukumbuke kuwa ili kijana awe na maendeleo mazuri shuleni na katika maisha yake ni lazima awe na heshima.

## Maswali

1. Baadhi ya watu huamini nini kuhusu hatima ya mtu maishani?
2. Taja maelezo ya hatima kulingana namwandishi.
3. Ni nini imani ya baadhi ya watu katika dunia ya leo?

4. Mafikira ya kutofanya chochote maishani yamewaathiri sana kina nani na yana madhara gani?
5. Kwa nini mwandishi anasema vijana wengi hawana utaratibu maishani?
6. Kulingana na kifungu vijana wana picha gani juu ya shule?
7. Taja vitendo hasi ambavyo vijana wanafanya shuleni.
8. Taja baadhi ya uhalifu unaotekelezwa na vijana wapotevu.
9. Kulingana na kifungu wanafunzi wa kidato cha kwanza wandhulumiwa vipi?
10. Eleza kupotoka kwa wasichana kimavazi.
11. Ni nini kinachowavutia wasichana kwa mahusiano na wazee?
12. Taja athari ya dada watalii kwa dada zetu.
13. Je, wavulana wameathiriwana usasa? Thibitisha.
14. Mwandishi analaumu nani kwa kupotoka kwa vijana?
15. Eleza vile vijana wanatumia mitandao visivyo.
16. Mwandishi anawapa vijana taadhari ipi kutokana na ujana?
17. Ujana unapaswa kutumiwaje kulingana na mwandishi?
18. Taja makundi mawili yanayopaswa kuongoza vijana kulingana na mwandishi.
19. Kulingana na aya ya mwisho vijana wanapotoka kwa nini?
20. Ni jambo lipi ambalo litamfanikisha kijana maishani kulingana na aya ya mwisho?

**Kifungu b**

## Wosia kwa vijana na wazazi

Vijana, tuache kuona ugumu kwenye kila tatizo na tuanze kuona fursa.Dira ya taifa lolote ipo mikononi mwa vijana. Wao ndio wanaoweza kuitabiria nchi yao itakuwa wapi katika kipindi fulani, iwe ni malengo ya muda mfupi au mrefu.

Wao ndio wenye nguvu ya kufikiri. Kutakuwa na matumizi ya chini ya rasilimali iwapo hawatapewa nafasi ya kutumia vipawa vyao kulijenga taifa.

Wajibu wa taifa ni kuwapa elimu nzuri vijana ili wawe raia wenye manufaa siku za usoni. Wajue kusoma, kuandika, kudadavua na kuzungumzia maslahi ya taifa lao kwa kina. Mafanikio ya taifa yanawategemea vijana.

Yote kwa yote kila kijana anaota kuwa na nafasi fulani siku moja, lakini wenye kutoka nje ya mipaka ya utulivu, ndio watakaoweza kufanikisha ndoto zao.Wapo wanaotamani kuwa madaktari, wajasiriamali, wanasayansi na hata marais katika nchi zao.Hata hivyo, vijana hawatakuwa na manufaa kama watashiriki katika matendo yoyote yanayorudisha taifa nyuma.

Kila changamoto unayokumbana nayo kwenye maisha yako mwenyewe ni fursa kubwa katika namna ya kuifikia ndoto yako, cha kufanya ni kitu kimoja ni kubadili mtazamo na kuanza kutatua changamoto zote za kwako na zinazokuzunguka.

Tuache kuona ugumu kwenye kila tatizo na tuanze kuona fursa ndani ya changamoto tunazokumbana nazo au kuishi nazo karibu.Kwa mfano changamoto za uchafu barani Afrika ni kubwa lakini hii tunaiona kuwa fursa ya sisi kuitatua na kujipatia kipato. Vijana tunaouwezo wakuunda makundi tukawa tunakusanya uchafu nyumba kwa nyumba na mwisho wa siku tunatengeneza kipato kikubwa lakini tumetatua shida ya uchafu.

Vijana wengi wanaogopa kujaribu na kufanya baadhi ya mambo wakihisi watakosea. “Nitaonekana sijui, watu wengine watanionaje nisipofanikiwa?” ni baadhi ya maneno ya kutisha ambayo hujisemea ndani.

Ndoto zetu na mipango inakufa kwa sababu ya uoga. Labda kwa sababu wengi wetu tulilelewa hivyo kila kitu mpaka wazazi au walezi wakuruhusu, ukitaka hata kubadilisha nguo utotoni ilikuwa mpaka umuulize mlezi au mkubwa wako. Hii imetujengea hali fulani kubwa ya kutokujiamini katika uamuzi na kuwa na fikra za vijana.

Jitenge na vijisababu vya kusema “kwetu sisi maskini, mimi sijasoma, mimi siwezi, mimi kwetu hatujafanikiwa”. Sema hapana, songa mbele, kimbiza malengo na ndoto bila kuangalia visingizio vya aina yeyote.Ndoto, malengo na mafanikio yetu yapo mikononi mwetu. Pambana kwa kuwa wewe ni mshindi. Acha kuwa muoga. Uoga wako umasikini wako.

Kila mtu anapitia changamoto mbalimbali katika kutimiza ndoto na malengo yake kadha wa kadha katika maisha. Changamoto hutujenga kuwa watu wapya. Usione uko peke yako kwenye changamoto za leo, mwingine ana changamoto tofauti ambazo hutuandaa kuwa watu wenye mitazamo tofauti kabisa kulinganisha na hapo. Changamoto hubadilisha kesho yetu.

Ikiwa wewe ni mzazi au mlezi lazima kuna kipindi unapata hofu na mtoto wako ambaye unaona anaelekea katika rika la ujana na kepuvuka.Unafikiria mambo mengi ambayo wewe unayafahamu kama changamoto katika maisha ya ujana ambayo uliyapitia, na unaona kabisa na yeye sasa anaenda kukumbana nayo.Hofu yako kubwa ni, hujui atatumia njia gani kukwepa mitego ya jamii na kama ataingia kwenye mtego na kunaswa atatokaje?

Kiuhalisia kijana wako anapoanza kuchangamana na vijana wengine wenye historia mbalimbali huwa katika uwezekano wa kuiga tabia zao kwa kuwa anatumia muda mwingi kuwa nao kuliko wewe.Ushahidi unaonyesha kuwa vijana wengi ambao walikuwa wanapewa usia wa mambo ya maisha na wazazi wao,walivyofanikiwa kukwepa mitego hiyo kwa kukumbuka maneno ya mzazi, na hofu ya kutotaka kwenda kinyume na maelekezo yao.

Kuna kipindi wewe mzazi  au mlezi unaona kabisa kijana wako anaonyesha mabadiliko ya tabia,lakini unaona aibu kukaa naye chini na kumpa ukweli wa mambo ulivyo.Lakini waswahili wanasema;"Samaki mkunje angali mbichi"Ukishamkosea katika rika hili,basi uombe,awe na uzoefu binafsi wa kutambua vitaviliyo mbele yake ni vya namna gani na vipi atavishinda.

Kuna mambo saba ambayo mzazi unapaswa uanze kuzungumza na kijana wako:

1. Ngono na jinsia

Kijana wako, ambaye anakua atakutana na taarifa nyingi sana kuhusu ngono na jinsia ambazo nyingi sana huko mtaani huwa si sahihi, iwe kupitia vyombo vya habari au uzoefu atakaokutana nao yeye mwenyewe.Anza kuzungumza naye kuhusu masuala ya uzazi, mimba za utotoni, na utoaji wa mimba huku ukijikita katika madhara na namna ya kujikinga navyo.

2. Dawa za kulevya na pombe

Vijana wanapenda sana kuhudhuria burudani wanapokuwa mtaani, shule au hata vyuoni miaka ya mwanzoni.Huko wanakuwa katika hatari ya kutumia vileo kwa kuwa wanakutana na vijana wenzao wenye historia tofauti tofauti. Iwapo hutamnyoosha mapema wewe mwenyewe vijana wenzake watamnyoosha katika njia zao.Wengi wao wanaingia katika mkumbo kwa kuwa, hawakupata taarifa sahihi kutoka kwa wazazi wao juu ya madhara ya tabia hizo,na pia kukwepa kuonekana mshamba.

3. Matumizi ya pesa
Kipindi cha ukuaji mahitaji na matumizi ya kijana yanaongezeka kwa kasi kubwa sana, hata kutunza kidogo anachopata kwake huwa ni tatizo. Zungumza na kijana wako umuonyeshe namna ya kutunza kidogo anachopata.Mueleze faida za kutunza pesa zilivyo na zitamsaidiaje katika maisha yake ya kujitegemea.

4. Umuhimu wa familia
Mara nyingi, vijana wanapopata nafasi ya kufanya shughuli zao wenyewe, kukaa karibu na familia huwa ni kitu kigumu.Hata muda anaotumia kukaa na wanafamilia wenzake huwa ni mdogo kuliko anaotumia kukaa na marafiki.Tumia busara zako kumuunganisha na wanafamilia wengine ili washirikiane pamoja.

5. Mahusiano
Vijana hawaoni tabu kubadilisha marafiki hata kwa mwezi mara nne na bado akajiona yuko sawa kwa kuwa anawabadilisha anavyotaka.Usimruhusu kijana wako awe na misingi isiyostahili, kwani itakuja kumuumiza siku zijazo.Nawe hautajivunia utakapokuwa unayasikia na kuona kumhusu yeye.Kaa naye kabla hajaingia huko,na ujaribu kumuongoza katika njia sahihi za mahusiano.

6. Matumizi ya mitandao



Katika zama hizi ambazo teknolojia ya mtandao wa intaneti imeenea kila mahali vijana wamekwamia hapo kama wamewekewa gundi. Kinachopaswa ni wewe mzazi kumfundisha mambo yapi   yana umuhimu na yapi hayana umuhimu kwake katika mtandao wa intaneti mapema, sio mpaka ulimwengu wa nje uje umfundishe akiwa ameshaumia.

7. Tafsiri ya kufanikiwa

Vijana wengi,tuna tafsiri tofauti tofauti juu ya maana halisi ya kufanikiwa katika maisha.Hapa ndipo tunapoanzia kupoteza dira kwa sababu tunayoyahangaikia kwa kudhani ndio yatakuwa mafanikio yanakuja kuwa sio.Iwe katika michezo, elimu, au jambo lolote ambalo litakuwa linahusisha nguvu na akili zake lazima umpe tafsiri sahihi ya kufanikiwa ni kuwa na nini.Yafuatayo unaweza ukaanza kuyafanya leo:Mpe usalama,muonyesha upendo na kumjali,weka misingi yako ambayo yeye ataifuata kipindi yupo chini yako,muadhibu pale inapobidi,kuwa na muda wa kutosha kukaa naye na kuzungumza naye, fuatilia uhusiano wake na wengine, muonyeshe mfano.

Kila mzazi anapenda kuona mtoto wake akiwa anajihusisha na mambo ya msingi katika maisha yake. Ukianza kumtegenezea mazingira hayo tangu mapema utaweza kujivunia tabia yake ya kesho.Isije baadaye kijana wako

akakulaumu kwamba hukumueleza na kwamba umechangia kuharibu maisha yake kwa kukaa kimya.

## Maswali

1. Vijana wanashauriwa nini juu ya shida za kila siku?
2. Ni nini mwandishi anawasihi vijana kuhusu nchi yao?
3. Taja madhara ya kutowapa vijana nafasi ya kuendeleza vipawa vyao.
4. Taja vitu vinne ambavyo tungetaka vijana wapate kupitia kwa elimu.
5. Kulingana na mwandishi ni vijana wepi ambao watanufaika na ndoto zao?
6. Taja taaluma tatu ambazo mwandishi anazitoa kama mifano ya ndoto za vijana.
7. Vijana wanawezaje kunadhifisha mazingira kulingana na kifungu?
8. Taja baadhi ya hofu za vijana katika kutimiza ndoto zao.
9. Malezi yanaweza kumtia kijana woga wa uamuzi. Thibitisha kulingana na kifungu.
10. Eleza visingizio ambavyo kijana anapaswa kuviepuka ili kuendelea maishani.
11. Changamoto tunazopitia katika maisha yana umuhimu wowote?Thibisha kwa hoja mbili.
12. Wazazi wanaofia wakati upi wa watoto wao?
13. Ni nini ambacho mzazi anahofia kwa wakati sana?
14. Kutangamana kwa vijana kuna athari ipi?
15. Ni njia ipi inayoweza kumwokoa kijana kutoka kwa athari za kutangamana?
16. Ni nini kinaweza kumzuia mzazi kumwelekeza mtoto wake akiona mabadiliko?
17. Mzazi asipomuonya mtoto kwa wakati mtoto anaachiwa jukumu gani?
18. Taja njia mbili ambazo vijana wanapata maswala ya ngono.
19. Kulingananakifungu, taja mambo ya ngono ambayo mzazi anapaswa kumwambia kijana wake.
20. Taja mandhari matatu ambayo kijana anaweza kuanza kujifunza ulevi.
21. Ainisha sababu mbili zinazowafanya vijana kuingia katika ulevi.
22. Ni nini umuhimu wa kufunza kijana matumizi mwafaka ya pesa?

23. Kwa nini kwa wakatimmoja vijana hawataki kukaa na wanafamilia?
24. Mzazi atafanyeje kuhakikisha kijana hajitengi na familia?
25. Mwandishi ametaja shida ipi ya mahusiano ya vijana?
26. Jukumu la mzazi ni lipi katika mahusiano?
27. Taja jukumu la mzazi katika matumizi yakijana wake ya intaneti.
28. Ni nini kinawafanya vijana kupoteza dira ya maisha?
29. Ufanisi maishani wa kijana unahusu mzazi.Ni mambo yepi ambayo mzazi atamwelekeza kijana ili afanikiwe?
30. Mzazi anapaswa kuepuka lawama ya mtoto wake. Thibisha haya kulingana na aya ya mwisho.

## Kifungu c
## Uamuzi maishani

Katika Maisha yetu ya kila siku mara nyingi tunajikuta katika mazingira yanayotulazimu kufanya maamuzi magumu au kuchagua kitu kati ya vitu vingi ambavyo vinatuchanganya akili. Wengi wetu kwa ugumu huu wamejikuta wakifanya maamuzi mabaya na kuchagua chaguzi mbaya ambazo ama ziliwapa hasara au ziliharibu kabisa mwelekeo au mustakabali wa maisha yao. Maisha nijinsi unavyofanya maamuzi.Tunapofanya maamuzi fulani, hususani katika kuchagua vitu kati ya vingi, hatumaanishi vyote au vile vingine ni vibaya bali hatuwezi kuvichagua vyote kwa wakati mmoja na hivyo tunalazimika kufanya maamuzi ya kuanza na kimoja na kumalizia na vingine.

Kuna mbinu tofauti ambazo zitakuwezesha kufanya maamuzi yako kwa haraka, kwa ubora na bado ukawa katika uwezo wa kuyasimamia maamuzi hayo.Kwanza,angalia na zitafute fursa mbalimbali; jambo la kwanza ni uwezo wa kuzidaka fursa pale zinapojitokeza. Katika jambo la kwanza, la uwezo wa kuzidaka fursa, ina maana kuwa, baada ya kueleza au kutangaza kwa marafiki na kupitia njia mbalimbali kuwa unataka kutafuta kitu au kazi fulani, haupaswi kukaa tu kimya na kulala, fursa zaweza kuja kupitia marafiki zako, wafanyakazi wenzako, au kupitia matangazo uliyoyafanya maeneo mbalimbali, sasa hapa haustahili kulala bali kuzidaka na kuzifanyia kazi fursa hizo.

Jambo la pili ni uwezo wa kuzitengeneza fursa wewe mwenyewe.Katika jambo la pili, kama kweli unahitaji kitu lazima ufungue macho kutafuta nini tatizo la jamii inayokuzunguka, wakati wote tatizo au hitaji la jamii laweza kugeuzwa kuwa fursa. Mfano, kama sehemu ni kame na maji ni tatizo jitahidi kuchimba kisima, kwa kutatua tatizo lililosumbua jamii umepata fursa ya kufanya biashara. Usikae tu na kusubiri fursa zijikabidhi miguuni pako zenyewe. Kimbia uzinyate.Njia zote hizi mbili hazinabudi kutiliwa mkazo na kila mtu.

Jizindue wewe mwenyewe; uzinduzi una maana kuwa tendo la kuchukua na kuuendelea na mkondo uliouchagua ili ukutoe kimaisha. Fanya uzinduzi wako mwenyewe bila kusubiri ufanyiwe. Ili kuweza kujizindua pasipo kuchelewa, lazima kufuata ushauri ufuatao.

Ili kufanikiwa, kila wakati jiulize ni nini unachotaka kukifanya na katika hiki unachotaka kukifanya, ni nini unachotaka kukipata?Unaporuhusu akili yako kufahamu ni nini unachotaka kukipata, unauruhusu mwili na nafsi yako kujitia nguvu tayari kwa kukiendeleza hicho kitu.Faida nyingine ya kujiuliza ni nini ninachokitaka ni kukupa picha ya ukubwa au umuhimu wake.

Kufanikiwa maishani ni lazima uwe tayari kupata hasara! Kama wewe ni mwoga wa kushindwa au mwoga wa kupata hasara kamwe hutoweza kujizindua kwa haraka. Kwa ajili hii lazima ujue jinsi ya kushughulikia hizo hofu zako. Usiogope kupata hasara katika chochote ufanyacho maana kupitia hasara tunajifunza mbinu bora zaidi za kuitafuta faida kubwa.

Jifunze kutumia vyema na kwa ufanisi maamuzi yako**.**Kwa mfano,jifikirie umebeba gilasi tupu mkononi mwako, waweza kuijaza gilasi hiyo kwa majuto na lawama za uliyowahi kuyafanya au waweza kuijaza kwa yale uliyojifunza huko nyuma kwa ajili ya kesho yako. Kama utabaki kujuta na kulaumu yaliyopita au uliko sasa hutofaidika chochote kiujuzi kwa ajili ya kesho yako. Lakini kama utafanya kila utakalokumbana nalo kuwa ni somo utapata ujuzi tele kwa kesho yako.

Pinga tabia ya kulaumu na kujutia maamuzi yako kwa kuzingatia ukweli kwamba mambo mengi hutokea au hutegemea mitazamo uliyo nayo.Maamuzi

mengi tufanyayo hutegemea mitazamo tuliyonayo maishani.  Kama mtazamo wako ni wa kujutia kila kitu au kulaumu wengine, basi utalaumu na kujutia kila utakachowahi kukifanya, mfano; utajutia na kulaumu kozi unayosoma, kazi unayofanya, biashara unayofanya, mke au mume mliyeoana naye, watoto uliowazaa na mengineyo.

Maamuzi ufanyayo yanategemeana sana na mfumo wako wa maisha. Maamuzi yako maishani hutegemea sana na kile unachokiamini. Kile ulichotayari kukisimamia na kukitetea, hutegemea sana uasili wa maadili yako, kupitia hivi vitu tunapata maamuzi mabaya au maamuzi mazuri. Mfano, maamuzi ya mtu mwenye maaadili ya kidini ni tofauti na maamuzi ya yule asiye na dini.
Jifunze kufanya uamuzi; jitahidi kuweka misimamo na malengo sahihi katika maisha yako.Jaribu kuwa na msimamo fulani badala tu ya kuelea elea tu hewani ukisubiri wengine wakusaidie kuamua.Jitahidi kuyatetea na kuyasimamia maamuzi uliyofanya.Yathibitishe maamuzi yako kabla hujaamua kuyaacha na kufuata maamuzi mengine.




Wakati tunapofanya uamuzi wowote tunazifutilia mbali fursa nyingine zozote na kuchukua ile tu tuliyoiamua.  Fahamu dhahiri kuwa uamuzi wakweli unamaanisha kujitoa, kujifunga katika lile ulililoliamua.

Sio wakati wote maamuzi tunayoyafanya yanatufikisha pazuri au kutuletea matokeo mazuri.  Mara nyingine unajikuta mara tu ulipoamua kujizindua mwenyewe, maamuzi hayo yanakutupa kwenye hasara au majuto. Unafanyaje hili linapotokea? Amini ujasiri wako.Ni kosa kubwa sana kujikosoa

na kujisuta na kuusuta ujarisi uliokuwanao mara tu baada ya kujiona umefanyakosa. Fahamu kwa wakati wowote unapofanya jambo la kijasiri kuna mambo mawili, labda upate matokeo mazuri au upate matokeo mabaya. Lakini, kupata matokeo mabaya kwa sasa hakubadili ukweli kwamba kile kilichofanyika kilifanywa kwa ujasiri.

Katika hali zote ni vizuri kuchukua masomo yaliyo muhimu katika changamoto za maisha.Katika kila hali tunayopitia hakuna cha kuacha kisichokuwa shule nzuri itakayo kusaidia kesho. Jifunze kuyatazama mapito magumu kama darasa la kujifunza kustahimili kesho, yamkini isiwe shule itakayokusaidia wewe, lakini kwa kuyajua hayo uliyijifunza utawakwamua wengi watakao kwama katika tope linalo fanana na lakwako kesho.

Maisha ya mwanadamu siku zote yanaongozwa na maamuzi anayoyafanya kila siku. Yapo maamuzi ambayo ukiyafanya yanakupelekea moja kwa moja kwenye kufanikiwa au kushindwa. Kwa hiyo hali yako uliyonayo sasa inategemea na maamuzi uliyoyafanya wewe siku za nyuma.Kama ulikuwa mtu wa kufanya maamuzi mabaya basi maisha yako nina uhakika sio mazuri kwa sasa. Je, unajua ni maamuzi gani unayotakiwa kuyafanya ili kubadili hali yako ya sasa na kuwa na mafanikio makubwa? Kwanza amua kuwa makini na kile unachokizingatia.Mara nyingi kile unachokizingatia kila wakati, kila mara na kila siku ndicho kinachoamua maisha yako ya leo na baadaye yaweje. Kama wewe mawazo yako kila wakati yamejikita katika tabia mbaya ambazo sio za kimafanikio zitakusababishia kuwa si rahisi sana kuweza kufanikiwa na kubadili hali yako kwa sasa.

Wengi wanaoshindwa kubadilisha hali zao walizonazosasa, utakuta ni watu ambao kiuhalisia wanazingatia sana mambo yanayowatoa nje ya mstari wa mafanikio. Mambo hayo yanaweza yakawa ya kupoteza muda, kutojisomea, kutokujiwekea malengo na mengineyo. Hivyo, ili uweze kufanikiwa ni lazima kufanya uamuzi wa kuwa makini na kile unachokizingatia kila wakati.

Uamuzi mzuri ni ule wa kuamua kuwekeza. Haijalishi unapata pesa nyingi kiasi gani kwenye kile unachokifanya ila kama bado hujaamua kuwekeza zaidi na zaidi, basi hali yako ya kipato itabaki vilevile siku zote. Amua kuwekeza katika

mambo mbalimbali ambayo yatakufanya uendelee na kuwa mshindi katika maisha yako. Hebu jaribu kuangalia, akina nani ambao ni watu wenye mfanikio makubwa? Utagundua ni wale tu ambao maisha yao wameamua kuwekeza kwa hali na mali.

Amua kubadili mfumo wa matumizi yako.Unaweza ukawa unapata kweli pesa ya kutosha inayoweza kukusaidia, lakini kama bado mfumo wako wa matumizi ni mbaya basi sahau kuweza kufanikiwa. Wengi mara nyingi wanaangushwa na matumizi yao mabaya ya pesa. Wanakuwa ni watu wa kutumia wakati mwingine hata nje ya kipato chao wanachokipata.

Ili uweze kufanikiwa na kuboresha hali yako ya kipato kwa namna yoyote ile ni lazima uwe makini sana na kile unachokitumia. Umakini huu utakupelekea wewe kutunza pesa nyingi ambaza zingeweza kutumika ovyo bila sababu ya msingi. Ili uweze kufanikiwa na kubadili mfumo wa matumizi yako, jiwekee bajeti ya kukuongoza katika hilo.

Ukifuatilia kidogo tu, utagundua kwamba watu wenye mafanikio makubwa mara nyingi ni watu wa kuchukua hatua za kubadili "masiha" yao kila siku. Hawa sio watu wa kukaa na kusubiri hali fulani ziwatokee, ni watu wa vitendo. Kwa vitendo vivyo hivyo huweza kuwafanikisha. Huu ni uamuzi wa lazima kuuchukua ili kuboresha hali yako ya kipato.

Hayo ndiyo maamuzi ya msingi unayoweza kuyafanya leo na kubadili hali yako ya kipato na kuwa mtu wa mafanikio. Kila kitu kinawezekana kwako ukiamua kuchukua hatua.

## Maswali

1. Kulingana na aya ya kwanza uamuzi ni nini?
2. Kulingana na mwandishi uamuzi bora ni upi?
3. Hatua ya kudaka kitu inahusisha nini?
4. Baada ya kuamua unataka kitu nafasi zinaweza kupitia wapi?
5. Mwandishi anaposema lazima ufungue macho unapokitaka kitu anamaanisha nini?
6. Kulingana na kifungu uzinduzi ni nini?

7. Kufanikiwa maishani ni lazima uwe tayari kupata hasara.Thibitisha kulingana na kifungu.
8. Gilasi iliyo tupu inafunza nini katika maisha?
9. Mwandishi anasema kama maisha yako ni ya kujutia utajutia vitu fulani.Vitaje vitu hivyo.
10. Imani katika dini ina nafasi yoyote katika uamuzi wa mambo yako? Thibitisha kulingana na kifungu.
11. Mapito magumu yanatufunza nini katika maisha?
12. Maisha ya binadamu yanategemea nini kulingana na kifungu?
13. Maamuzi ya mtu katika maisha yanaweza kumpelekea kwa mambo mawili.Yataje
14. Maisha yako ya sasa yanategemea nini?
15. Matatizo yako yawafaidi wengine kwa njia gani?
16. Ni uamuzi upi wa kwanza unaopaswa kufanya ili ufanikiwe?
17. Taja mambo matatu yanayoweza kumpotezea mtu mstari wa mafanikio.
18. Ni nini umuhimu wa kuwekeza pesa?
19. Kulingana na kifungu watu ambao wamefanikiwa wameweza kufanya nini?
20. Kwa maoni yako ufanisi maishani unategemea nini?

## Kifungu d:
## Kukata tamaa

Vijana wengi wako katika tandabelua la kukata tamaa.Wengi wahisi kuwa dunia imewachenga hivyo wameishia kukata tamaa.Swali la kwanza ni,kukata tamaani nini? Kukata tamaa ni hali ya kupoteza matumaini. Hali hii hutokea pale ambapo mtu amepoteza wazo au matumaini ya kufanikiwa katika matarajio yake ya kupata kitu fulani au kufanikiwa kwa jambo lolote alilopanga kulifanya. Pia ni kupoteza tumaini la kufikia malengo katika jambo fulani alilopanga kulifanya au analolifanya**.**Ni hali inayoweza kutokea katika mfumo wa maisha ya kila siku, iwe nyumbani, kazini, shuleni, kwenye biashara, katika mahusiano au mahali pengine popote katika mfumo wa maisha.

Kukata tamaa ni hali ya kufikia kikomo juu ya mafanikio ya jambo halisi. Kufikia kikomo huko hutokana na kujenga taswira na hoja ya kushindwa katika mawazo yako juu ya suala lolote ulilopanga kulifanya au unalolifanya. Ni hali ya kuchoshwa au kuvunjwa moyo kunakotokana na mtazamo hasi unaoweza kuujenga baada ya kufikia kikomo wa ufahamu, ufumbuzi au jawabu la suala lolote linalokukabili, iwe kutokana na mawazo yako binafsi au mawazo yatokanayo na watu wengine.

Zipo dalili nyingi za mtu aliyekata tamaa ambazo zinaweza zikawa zinatofautiana kutokana na mazingira, sababu, wahusika, matukio na mengineyo. Lakini zipo dalili za msingi na za jumla kwa watu wote. Dalili hizo tunaweza kuzigawa katika sehemu mbili kuu ambazo ni: dalili za ndani na dalili za nje. Dalili za ndani ni dalili ambazo watu wengine nje ya mhusika hawawezi kuzitambua kiurahisi, ni muhusika tu ndiye anaweza kuzitambua au kuhisi.Baadhi ya mambo ambayo yanaonyesha dalili za ndani ni kama vile kukosa msukumo kimawazo.Kila jambo linaanzia kwenye mawazo,na ili mtu afanikiwe anahitaji msukumo ambao ni ushawishi wa mawazo. Maana mawazo anayokuwanayo mtu kwa muda mrefu huwa yanajitokeza katika maneno yake na hatimaye katika matendo yake. Hivyo basi ukiona msukumo wa mawazo yako ya mwanzo umepungua, basi ujue kuwa hiyo ni dalili mojawapo ya kukata tamaa.

Dalili nyingine nikuhisi kuchoshwa kimawazo na kila kitu au kila mtu.Ukiona mawazo yako yamechoshwa kwa kuliwazia jambo fulani ambalo mwanzoni ulikuwa umelipanga vizuri au kila mtu unamwona kama mzigo kwako, hiyo ni dalili ya kukata tamaa.

Kukata tamaa huonyeshwa na dalili ya mawazo ya kushindwa au mawazo hasi. Haya ni mawazo ambayo siku zote hayana ushawishi wa kukusaidi kufanya jambo lolote, badala yake huleta woga wa kufanya jambo kwa kuhofia kushindwa au kukosa uhakika wa kufikia malengo.

Kukosa ubunifu wa njia mbadala**;** ukiona jambo linashindikana kwa njia moja na huku unakosa ubunifu wa njia mbadala jinsi ya kulifanikisha jambo hilo, nayo inaweza ikawa ni dalili ya kukata tamaa. Kila mtu ana uwezo mkubwa sana wa ubunifu, tofauti zetu zinajitokeza pale ambapo wengine wanashughulisha sana

sehemu ya ubongo zinazo husika na ubunifu, wakati wengine wamezilemaza.Ukilemaza ubongo, unakosa ubunifu wa njia mbadala.

Wakati mwingi mtu ambaye amekata tamaa hupoteza furaha au hamu ya jambo husika.Jambo ambalo ulikuwa unalifurahia na kuliona nzuri, huku ukifikiria kufikia mafanikio, ghafla unaanza kupoteza furaha au hamu ya jambo hilo.Dalili hii huandama na kutofurahia ushauri.Mara mtu anaanza kuchukia ushauri hasa unaokwenda kinyume na mawazo yake au ushauri unaokushawishi kuendelea kufanya jambo ambalo umeamua kuliacha.Mambo yakiwa hivyo basi utakuta mwathiriwa anafanya maamuzi ya haraka.Mawazo yake yanapoamua kufanya maamuzi yanayohatarisha maafanikio yake, au kuhatarisha maisha yake kama kujiua.Baadhi ya watu hutamani kufa kuliko kuishi kwasababu ya mambo ya hapa duniani yaliyowaumiza mioyo.Wengine hutamani kujiua na wenginehufikia hatua ya kumwomba Mungu awachukue.

Mara nyingi mhusika hujihurumia. Hili nalo ni tatizo la ndani ya mtu, kujihisi hufai kabisa, unahisi maisha yako hayana jambo lolote la maana la kuchangia na hayafai kabisa.Huenda ukahisi unahatia nyingi.

Dalili za nje ni dalili ambazo watu wengine nje ya mhusika tunaweza kuwa mashahidi kwa kuziona kwa uwazi na kutambua kwamba mwenzetu amekata tamaa. Kwa mfano mtu aliyekata tamaa, huwa na maneno yanayoashiria kukata tamaa, maneno yanayokiri kushindwa. Ukimsikia mtu anazungumzia jambo linalohusu kufanikiwa au kutofanikiwa katika maisha, na kama anayasema hayo kwa hiari yake mwenyewe, basi chunguza, utagundua hayo ndiyo mawazo ya moyo wake.

Vitendo vinavyoashiria kukata tamaa ni pamoja na mambo yanayoongoza kwa kuongeza vitendo vya utovu wa maadili, Mfano utumiaji wa dawa za kulevya, ukahaba na mengineyo.

Mabadiliko ya tabia mara nyingi, toka tabia nzuri kwenda tabia mbaya, hutokana na kukata tamaa. Tena mara nyingi mabadiliko ya tabia yanapotokea huwa yanatanguliwa na matukio au sababu ya kukata tamaa.Mara nyingi mtu huanza tabia ya kujitenga au tabia ya kuwa peke yake, na kukosa furaha kwa mtu

ambaye tunajua kuwa alikuwa na hali ya kawaida. Ghafla anaanza kukosa furaha na kuwa mnyonge, inawezekana kabisa kuwa hiyo ni dalili ya kukata tamaa.Kwa wakati juhudi zake hupungua nahupoteza mwelekeo .Wakati mwingi mtu akikosa mwelekeo basi huchukua hatua zisizotarajiwa, kama vile hatua ya kujiua, au nyingine ambazo ni kawaida kutokea katika jamii.

Wakati mwingi watuhujikuta wakilia tu wanapokumbuka mambo magumu waliyopitia. Hii ni dalili ya kukata tamaa. Watu wengine ambao waliumizwa mioyo na wengine, mara wanapoelezea juu ya matukio yaliyowaumiza hujikuta wakipiga kelele za kulia.Kama vile moyo unapokuwa na furaha hudhihirika usoni mwa mtu, vilevile moyo unapokuwa na matatizo hudhiirika usoni mwa mtu. Kadri unavyolinda moyo wako ndivyo unavyolinda uso wako na maisha yako kwa ujumla.

Zipo athari nyingi za kukata tamaa na athari zenyewe ni Kutofikia malengo uliyojiwekea, kubakikatika hali yeyote ambayo kabla ulihitaji kujikwamua. Mfanoumaskini,maradhi,ujingakuchanganyikiwakiakilinauwezowa kokiutendaji. Sio rahisi kuepuka maradhi kama shinikizo la damu, madonda ya tumbo,kisukari na mengine yanayofanana na hayo kutokana na mfadhaiko.Vijana tuepuke kukata tamaa maishani kwani hasara zake ni nyingi sana, ishi maisha ya matumaini na furaha.

## Maswali

1. Eleza maana tatu za dhana ya kukata tamaa kulingana na kifungu.
2. Hali ya kukata tamaa hutokea lini?
3. Taja mazingira matatu ambayo mtu anaweza kukata tamaa kulingana na aya ya kwanza.
4. Dalili za kukata tamaa hutofautiana kulingana na nini?
5. Taja aina mbili za dalili za kukata tamaa.
6. Eleza maana ya dalili za ndani.
7. Eleza maana ya dalili za nje.
8. Msukumo wa mawazo ni nini?
9. Dalili ya kuchoka kimawazo inadhihirika kupitia mambo mawili.Yataje.
10. Mawazo hasi husababisha nini?

11. Unapolemaza ubongo wako kufikiria ni dalili ipi ya kukata tamaa inajitokeza?
12. Dalili ya kukosa furaha kama njia ya kukata tamaa ina dalili zingine.zitaje kulingana na kifungu.
13. Mtu anapohisi hafai anajilaumu kwa mambo yepi mengine?
14. Maneno ya mtu yanawezaje kuonyesha kukata tamaa?
15. Utovu wa nidhamu unaoashiria kukata tamaa ni upi?
16. Ni mabadiliko yepi ya tabia yanayoonyesha kukata tamaa?
17. Dalili ya kukata tamaa kwa kujitenga huandamana na mambo yepimengine?
18. Taja matukio mawili ambayo humpelekea mwathiriwa wa kukata tamaa kulia machozi.
19. Taja athari za kukata tamaa.
20. Ni magonjwa yepi yanayomfika mwenye kukata tamaa?

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

### Viunganishi

Viunganishi ni maneno yanayounganisha:

a) Wazo kwa wazo.
b) Kikundi kimoja cha maneno na kingine.
c) Sentensi moja na nyingine.
d) Kauli moja na nyingine.
e) Ujumbe mmoja na mwingine.

Mifano ya viunganishi: isitoshe, wala, lakini, pia, tena, sembuse, licha ya, ingawa, ijapo, lakini, kwa mfano, kwa maana, kwa sababu, tena, aidha, mbali na, kwa vile, hata, hadi, ila, au, hivi, kwa minajili ya, kama, kwamba, angaa, ili n.k.

## Aina ya Viunganishi

### a) Sababu

Viunganishi hivi hutoa sababu ya kufanyika au kutofanyika kwa jambo. Ni maneno kama vile ile, kama vile, maadamu, kwa minajili ya na kwa sababu.

*Mifano:*

1. Nilimwita ili nimjulie hali.
2. Alimsimamisha kazi kwa vile hakuwa mwaminifu.

### b) Uteuzi

Hutumika ili kuteua chaguo baina ya vitu viwili au zaidi. Mifano ni: aidha, wala, au, ama.

*Mfano:* Sikumtembelea wala kumpigia simu.

### c) Ulinganishi

Ni maneno ambayo hutumiwa kulinganisha kitu kimoja na kingine. Ni maneno kama vile: kuzidi, kefu, seuze, sembuse, kuliko n.k.

*Mifano:*

1. Alishindwa na mbio za masafa mafupi, sembuse kukwea mlima.
2. Chai ya maziwa ni bora kuliko kahawa ya maziwa.

### d) Viunganishi vya ziada

Hutumika kuonyesha nyongeza. Ni maneno kama vile licha ya, pia, pamoja na n.k.

*Mifano:*

1. Licha ya kufuga kuku, anafuga sungura.
2. Alimrudisha shuleni kisha akamlipia karo yote.

### e) Viunganishi vya tofauti

Huonyesha tofauti ya mambo mawili au Zaidi kwa kuyaunganisha. Ni maneno kama vile: ingawa, isipokuwa, ila, bali, hata hivyo, walau, lakini, ijapokuwa.

*Mifano:*

1. Ingawa nilimkaribisha kwetu, sikuridhishwa naye.
2. Mkumbushe kuosha nguo zake lakini usimsaidie kuziosha.

**Zoezi**

**A. Tambua viunganishi katika sentensi hizi.**

1. Alimbeba ijapo kwa shida.
2. Mwandikie barua angalau tujue iwapo alifika.
3. Chukua jembe, kisu pamoja na kifyeko.
4. Nimesafiri kwa ndege sembuse gari moshi.
5. Lau tungekubaliana, matatizo hayangetokea.
6. Alimpakulia chakula, isitoshe akampa malazi.
7. Atatrudi kesho kwa minajili ya kukuomba msamaha.
8. Aidha uchukue vifaa vyote au uachane navyo.
9. Simjui wala simdhamini.
10. Watafika kwa sherehe muradi usiwaitishe zawadi.

**B. Unganusha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi sahihi.**

1. Lopi ni mwalimu. Lopoi ni mkulima.
2. Sitafika hospitali kumwona. Nitamtuma kakangu.
3. Michezo ya raidha hujumuisha mbio. Hujumuisha ujenzi wa viungo vya mwili.
4. Sokoni kumejaa matunda mengi. Kumejaa maembe, tikitimaji, machungwa na fenesi.
5. Ningelijua, nisingelienda kwake.
6. Jikakamue kwa masomo. Maisha ni kujitegemea.
7. Yote nilimtendea. Hakunishukuru.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

1. Andika kisa kuhusu njia za kujipa matumaini maishani.
2. Andika mazungumzo kuhusu mwathiriwa wa dawa za kulevya na mhudumu wa akili.
3. Vijana wanaweza kujiendeleza kwa nyanja mbalimbali.Jadili.

SURA YA 2

# USAWA WA JINSIA

Mada Ndogo ya 1:

## Kusikiliza na kuzungumza

**Soma shairi lifuatalo.**

Ufike shuleni kwake, Ripoti usiziache,
Ujue sahibu zake, Maskani si wachache,
Ukiweza waalike, Akiwika hadi kuche,
**Unavyolea wa kike, Sawia na wa kiume.**

Akichelewa kufika, Mjulie usichoke,
Kiwa utamtandika, Fimbo isiongezeke,
Asiweze haribika, Tendekezo usitake,
**Unavyolea wa kike, Sawia na wa kiume.**

Unapompa mapeni, Jua atumia vipi,
Kiwa kalipa madeni, Zilobaki huendapi?
Madawa ya masakani, Unajua shingi ngapi?
**Unavyolea wa kike, Sawia na wa kiume.**

Lisemwalo mbona lipo, Kitakwimu kitetesi,
Mabarobaro nilipo, Ni kama wana kisasi,

Wanalewa kama popo, Na mzazi huna wasi,
**Unavyolea wa kike, Sawia na wa kiume.**

Waume kichwa cha nyumba, Yupo anayenipinga?
Ela za leo kasumba, Mabanati wajijenga,
Sitishi mtaikumba, Ikiwa mtawatenga,
**Sawia na wa kiume, Umlee na wa kike.**

**MASWALI**

1. Mshairi anaongea juu ya nani katika ubeti wa 1?
2. Kwa nini mhusika anayetajwa atandikwe?
3. Ubeti wa 3 unaonyesha kuwajibika kwa njia zipi?
4. Mzazi anaonywa juu ya nini kwa ujumla?
5. Taja mafunzo ya shairi.

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

## Kifungu a

Haki za kibinadamu zimefafanuliwa kama haki za asili kwa wanadamu wote, utaifa wao, makaazi yao, kitaifa au kikabila asili, rangi, dini, lugha, au hali nyingine yoyote. Haki imekuwa suala la mjadala mkubwa wa falsafa, na bado kuna ugomvi kuhusu nini kifanyike.

Katika Sudan Kusini, wanawake wanaleta jamii pamoja. Wanawake wanatumia uzoefu wao kama waathiriwa wa mgogoro wa kusaidia majirani na familia zao. Wao wanaongoza majadiliano kati ya jamii ili kukuza uponyaji na uaminifu. Wanawake wa Sudan Kusini wanahitaji msaada wa viongozi wao na jumuiya ya kimataifa ili kudumisha kasi hii.Rais waSudan kusini Salva Kiir Mayardit anaongoza kwa kupigania   kuheshimu kwa haki za wa wanawake. Kiongozi huyu anasisitiza kutupiliwa mbali kwa mila na tamaduni potovu.




*Rais wa Sudan Kusini Salva Kiir Mayardit*

Miongoni mwa matatizo ya kijamii yanayolikabili taifa changa la Sudan kusini, kubwa ni mtindo wa watoto wadogo kuolewa mapema. Licha ya kuwepo sheria za kuwalinda lakini sheria hizo bado hazifanyi kazi ipasavyo. Ndoa za watoto wadogo bado ni tatizo sudan Kusini.




*Akina mama Sudan Kusini*

Zaidi ya nusu ya wasichana wenye umri wa kati ya miaka 15 na 19 nchini Sudan Kusini wanaolewa mapema, ikiwa ni kwa mujibu wa utafiti wa serikali ya nchi hiyo. Wasichana ambao wanajaribu kupinga ndoa za lazima wanakabiliwa na mateso makubwa kutoka familia zao.

Katika kadhia ambazo zilifuatiliwa na shirika la kutetea haki za binadamu Ulimwenguni inaonyesha wasichana wanapigwa, kutolewa maneno machafu na kutishiwa kuwa wao ni mkosi au kupelekwa polisi ili kuwalazimisha kuolewa. Jamii za watu wa Sudan Kusini zinaona utamaduni wa kuwaoza watoto wadogo kama jambo la kufurahisha wasichana wao na familia zao.Inaonekana njia muhimu kwa familia hizo hujipatia utajiri kupitia vitendo hivyo vya kitamaduni vya kuhamisha utajiri wa wanyama, pesa na zawadi zingine kupitia malipo ya mahari. Lakini uhalisia ni tofauti na ilivyo, kwani wasichana hao wanaachishwa shule wakinyimwa haki ya kupata elimu.

Utafiti wa kiafya unaonyesha wasichana walioolewa wakiwa wadogo, wanakabiliwa na hatari kubwa wakati wa ujauzito na kujifungua, kuliko walioolewa wakiwa wakubwa. Serikali ya Sudan Kusini tayari imechukua hatua kadhaa kupambana na ndoa hizo, kwa kuweka sheria ambazo zinatoa umuhimu katika kulinda kuwaoza watoto na wanawake katika ndoa zao.

Kuna juhudi pia ya kuendeleza mpango wa wasichana kupata elimu hata kwa kutumia njia mbadala za kupata elimu ambayo inawawezesha wasichana, akinamama na watu wengine waliopata ujauzito na hawakuwa na njia ya kuendelea na masomo au wale ambao wamekatishwa masomo yao.

Kuna tabaka na hali ya kutoelewa sheria iliyowekwa kulinda haki za akina mama na wasichana lakini sheria hizo zinakabiliwa na kutokuwa na. Matokeo ya kushindwa huko, wanawake wengi na wasichana wanandelea kupata tabu na kuishi katika mazingira ambayo yanaendeleza mpango wa kuwaoza wasichana wadogo.

Ni muhimu kwa serikali ya Sudan kusini kuchukua hatua kwani, ndoa hizo zinakwamisha maendeleo ya kijamii, kielimu, kiuchumi, kiafya na usalama wa wanawake na wasichana wadogo katika familia na jamii zao.

Sauti za wanawake wa Sudan Kusini zimezuiliwa katika mazungumzo ya amani. Kwa mfano mazungumzo yaliyofanywa Januari 2014, wanaume kutoka vikundi vya kupingana ndio walioongoza meza ya amani katika mji mkuu wa Ethiopia wa Addis Ababa. Viongozi wa Serikali na waasi wanaibua mazungumzo mara kwa mara na kwa upande mwingine, amani. Kwa kila mzunguko mpya wa mazungumzo, sauti za wanawake zinabakia chini haziwakilishwi kwenye meza.Tunapaswa kusisitiza kwamba sauti za wanawake wa Kusini mwa Sudan zipewe nafasi sawa katika meza ya amani.

Serikali ya Sudan Kusini na washirika wa maendeleo wanapaswa kutambua na kushughulikia mambo ambayo huzuia uwezekano wa wanawake, kama vile unyanyasaji wa kijinsia, ukosefu wa afya, elimu na huduma zingine na mambo ya utamaduni ambayo hupunguza uwezekano wa wanawake. Kushughulikia usalama wa vurugu za Jinsia na virusi vya UKIMWI ni masuala muhimu kwa wanawake na wasichana Kusini mwa Sudan. Madhara ya kimwili, kisaikolojia, na kijamii yanaweza kuharibu imani ya wanawake, kuzuia harakati zao, na kuharibu uwezo wao wa kufikia uwezo wao wote. Unyanyasaji wa wanawake pia huongeza uwezekano wa wanawake kupatavirusi vya Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

Upatikanaji wa huduma ambazo ni Afya na Elimu ni adimu sana.Wanawake katika Sudan Kusini hawapati huduma za afya na elimu. Afya ya wanawake ni tatizo halisi. Katika vijiji vingi, wanawake wanakosa matibabu au huduma za afya wakati wa ujauzito. Hakuna kliniki, hakuna dawa, na hapana lishe.Wanawake hata wajawazito wanakaa kwenye hofu ya usalama. Serikali inapaswa kujenga kliniki na vituo vya afya, hasa katika maeneo ya vijijini na kutoa dawa na vifaa.Kuna lazima kuwa na wauguzi waliofundishwa na hospitali safi.

**Maswali:**

1. Taja majukumu ya mwanamke wa Sudan kusini katika jamii.
2. Rais wa sudan kusini amewajabika kwa haki za akina mama.Thibitisha kulingana na kifungu.
3. Wasichana wadogo wanadhulumiwa vipi kulingana na kifungu?Toa hoja tatu.
4. Ni nini nia ya kuwaoza wasichana mapema?
5. Thibitisha jitihadi za serikali kwa mtoto wa kike.
6. Taja madhara ya ndoa za mapema kwa wasichana wa sudan kusini.
7. Thibitisha ukosefu wahaki ya wanawake waliohudhuria mkutano wa 2014.
8. Taja huduma mbili muhimu zinazohitajika na wanake sudan kusini.
9. Wanawake wajawazito wanateseka vipi?
10. Wauguzi wanahitajika kuwa vipi kulingana na kifungu?

**Kifungu B**

Nchi ya Sudan Kusini ina makabila zaidi ya 64, kila moja ikiwa na utamaduni wake wa kipekee. Makabila haya yanategemea maeneo ya kijiografia, na wengi wameona mabadiliko ya taratibu katika urithi wao wa kitamaduni zaidi ya miaka.

Hata hivyo, kanda ya kusini mwa Sudan bado inajulikana kwa tofauti ya kitamaduni. Jukumu la utamaduni la wanawake lina athari zake katika maendeleo ya kusini mwa Sudan. Wanawake katika utamaduni wa Sudan, kwa ujumla, hawana majukumu ya mamlaka au umuhimu wowote ulioheshimiwa katika familia zao au jamii. Wajibu wao ni wa kuolewa na mtu aliyechaguliwa na familia nje ya mfumo wa mahari, mfumo unaohusisha wanawake kama bidhaa ya kununuliwa au kuuzwa. Wanawake wa vijijini Kusini mwa Sudan hawana sauti kuhusu haki zao wenyewe, na hawawezi kushiriki katika mchakato wowote wa kufanya maamuzi kuhusu wenyewe au familia zao.

Katika tamaduni hizi zinazoongozwa na wanaume, wanawake wanapaswa kuwa watiifu na kushughulikia familia zao na waume wao.Katika makabila mengine,

kama vile katika mikoa ya Dinka na Nuer, wanawake wanaonekana tu kama chanzo cha mapato kwa manufaa ya familia.

Madhara ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na uhamisho wa makazi yalimwathiri mwanamke wa Sudan Kusini sana.Mwaka 2005, Mkataba Mkuu wa Amani (CPA) uliwekwa saini mjini Nairobi, Kenya,ili kukomesha vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa miaka miwili kati ya kaskazini na kusini mwa Sudan. Tangu wakati huo, utamaduni wa kusini mwa Sudan umepata shida kutokana na uhamisho wa wakimbizi wa Sudan Kusini katika nchi jirani kama vile Uganda na Kenya, na pia katika ulimwengu wa magharibi ambako walitetea. Ingawa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sudan vilikuwa na matokeo mabaya katika kifo na mateso ya mamia ya maelfu ya watu, matokeo yake pia yameleta mtazamo mpya kwa watu waliokimbia na hivyo wakaweza kwenda kufuata elimu bila kujali jinsia yao.Kwa mfano, wale ambao waliishi katika maeneo ya mijini au nchini Marekani walitambuliwa kwa jamii ambazo wanawake hutendewa tofauti sana na ambayo mahusiano kati ya wanaume na wanawake au mume na mke wanahusishwa kugawana nguvu, wajibu na maamuzi. Wanawake wa Kusini mwa Sudan ambao walikwenda maeneo hayo walipata matokeo mazuri ya elimu kwao wenyewe, watoto wao na familia zao. Labda kwa mara ya kwanza, waliweza kutambua mila ya kitamaduni ambayo hapo awali ilikiuka haki zao za kibinadamu.

Kwa upande mwingine, wanawake hao wa kusini mwa Sudan ambao walikimbilia nchi nyingine waligundua tamaduni ambazo mwanamke hakutaka kulazimishwa katika ndoa lakini anaweza kuolewa na mtu aliyechagua mwenyewe.
Mwanamke kijiji cha Kusini mwa Sudan hupewa majukumu mengi sana yakiwemo kuangalia watoto na wazee wa familia "iliyopanuliwa", kutoa huduma zote za maisha ya nyumbani na ya kila siku na kusimamia uzalishaji wa chakula.

Cha kushangaza, wanawake wa kusini mwa Sudan ambao wameweza kupata elimu huwa wa kuzingatiwa sana, hata kwa wanaume wanaoishi vijijini. Wanawake kama hawa mara nyingi huja kutoka familia zenye ustadi ambao wanaweza kuwapa elimu bora na wana uwezo wa kushikilia nafasi za serikali, kuajiriwa kwa faida na kushiriki katika maamuzi.

Ukweli nikwamba mabadiliko ya kitamaduni juu ya wanawake yanahitajika katika kujenga jamii ya kisasa. Sehemu muhimu ya mabadiliko haya inahusisha elimu. Elimu itawawezesha wanaume na wanawake wa Sudan Kusini kushikamana na mtazamo mkubwa wa ulimwengu na utawahimiza wanawake vijijini kutetea elimu ya watoto wao. Kwa sasa, wanaume wa kusini mwa Sudan wanatambua athari chanya ya elimu ya wanawake juu ya kuboresha kijamii kiuchumi na maisha ya familia.

Ingawa inaweza kuchukua muda kwa kukubalika kwa kuenea kwa mabadiliko haya kutokea, mabadiliko yanahitajika. Jukumu la wanawake linapaswa kubadilishwa kutoka kwa wanawake wa kukaa nyumbani na watoto wao na kutunza familia kwa dhana mpya ambayo wanawake wanakuwa na uwezo wa kutumia akili zao, zawadi na vipaji nje ya mazingira ya nyumbani. Mabadiliko ya kitamaduni yanahitajika kusini mwa Sudan ili kuwa nchi inayopambana na uchumi wa dunia. Wanawake kusini mwa Sudan wanapaswa kufundishwa kuwa utaalamu wao katika fani mbalimbali utachangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya vijiji na maeneo ya mijini katika nchi yao mpya.

**Maswali:**

1. Makabila ya Sudan Kusini yanatofautianaje?
2. Usambazaji wa makabila haya hutegemea nini?
3. Waume wa kuoa huchaguliwa vipi Sudan Kusini?
4. Wanawake wa Sudan Kusini hawapewi nafasi ya uongozi. Thibitisha.
5. Onyesha dhuluma ya uamuzi wa ndoa kwa mwanamke wa Sudan Kusini.
6. Taja makabila mawiliyanayomchukua mwanamke kama bidhaa ya kuwanufaisha.
7. Wakimbizi wengi walienda nchi zipi?
8. Mkataba mkuu wa Amani ulifanyika wapi?
9. Mkataba mkuu wa Amani ulilenga nini?
10. Orodhesha manufaa mawili ambayo wanawake wakimbiziwalipata.
11. Ni majumu yepi ambayo mwanamkewa kijijini ametwikwa?
12. Je, kulingana nakifungu kuna wanawake wa sudan kusini ambao wamefanikiwa kielimu?
13. Elimu itasaidiaje jamii ya watu wa sudan kusini?

14. Mwanamke aliyesoma ameleta faida gani kwa familia yake?
15. Mwanamke wamabadiliko mapya anapaswa kuwaje?

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

### Usemi halisi

Usemi halisi huwa na maneno ya moja kwa moja ya mnenaji bila ya kubadilishwa. Mambo yanayojitokeza katika usemi halisi ni kama vile:

a) Alama za kunukuu (“ “) hutumika.
b) Alama ya kuulizia (?) na mshangao (!) hutumika.
c) Nyakati zozote kama vile wakati uliopita, wakati uliopo, wakati ujao,mazoea, hali timilifu hutumika.

Matumizi ya herufi kubwa kwa nomino isiyo halisi katika kauli ya usemi halisi hutegemea muundo wa sentensi, kwa mfano;

1. Babu alisema, “Njooni hapa niwahadithie hadithi”.
2. “Njooni hapa niwahadithie hadithi,” babu alisema.

Ikiwa usemi unaanza na mnenaji, koma hufuata baada ya kumtaja mnenaji halafu alama za kunukuu. Kisha anza usemi kwa herufi kubwa. Usemi unapofika mwisho, alama ya nukta huwekwa halafu alama za kunukuu za kufunga usemi. *Mfano:* Maria alisema, “Ninahisi njaa.”

Usemi ukianza na maneno ya mnenaji, alama ya kunukuu ya kufungua usemi(“) hutumika mwanzoni mwa usemi. Herufi kubwa pia huanzisha usemi kisha mwishoni mwa usemi alama ya koma (,)huwekwa kabla ya alama ya kunukuu (”) ya kufungia usemi. Baadaye mnenaji hutajwa na alama ya kikomo (.) kuwekwa.

*Mfano:* “Ninahisi njaa,” Maria alisema.

**Zoezi**

**A. Sahihisha sentensi zifuatazo katika usemi halisi.**

1. “Mimi nitakutembelea leo jioni,” Asha alimwambia rafikiye.
2. Mwalimu mkuu alisema,“Ikiwa kuna mwanafunzi ambaye hajapata vitabu aje kuniona.”
3. Beba! Beba! Beba! Leo bei ya bidhaa imepunguzwa,” mnunuzi alisisitiza.
4. “Washiriki wafuatao wanione baada ya ibada: Juma, Sarah,Deng, Rosa na Awel,”mhubiri alisema.
5. Mtoto alilia,“Mama wee! Nataka chakula.”

**B. Andika sentensi katika usemi wa kauli halisi.**

1. Mwanasiasa aliahidi wananchi ya kwamba angewaletea maji ya mfereji namatangi ya kuhifadhi maji.
2. Fundi wa viatu alimaka na kumweleza mteja wake kuwa yeye hushona viatuna sio nguo.
3. Mlezi aliwaeleza watoto kuwa siku iliyofuata wangeenda kutembelea mbugaya wanyama pori.
4. Askari alimwita habusu Nassa mara tatu na kumuonya kwambahangemuonya tena.
5. Wavulana walidai ya kwamba walitaka usawa baina yao na wasichanawenzao.
6. Salaale! Kwa nini unamtusi mwenzako hivyo? kijana alimaka.
7. Mwalimu mkuu alisema, kesho sitaruhusu mwanafunzi kuhudhuria masomobila kumleta mzazi wake kwanza.
8. Susana! Susana! Nakuita mara ngapi? sisi tunaondoka leo Maria alisema.

## Usemi taarifa

Usemi wa taarifa ni usemi wa kuripoti yale yaliyosemwa na mnenaji. Huripotiwa bila kunukuu. Mambo muhimu yanayozingatiwa katika kauli ya usemi wa taarifa ni kama;

a) Alama za kunukuu (“ ”) hazitumiki.
b) Alama ya kiulizi (?) haitumiki.
c) Alama ya hisi (!) haitumiki

Baadhi ya vipengele hubadilika ifuatavyo:

**a) Nafsi ya kwanza na pili hubadilika na kuwa ya tatu**

**Mifano:**

1. Sisi tunapenda kulima, "mkulima alinena".
   Mkulima alikiri ya kwamba wao walipenda kulima.
2. "Nyinyi mtafagia nyumba," mama alisema.
   Mama aliwaambia kuwa wao wangefagia nyumba.

**b) Viashiria vya kwanza hubadilika**
**Mifano:**

1. Kiti hiki ni changu, "mwanafunzi alisema."
   Mwanafunzi alisema kwamba kiti hicho kilikuwa chake.
2. "Mgeni huyu ametutembelea," Jirani alieleza.
   Jirani alieleza kuwa mgeni huyo alikuwa amewatembelea.

c) **Viwakilishi vya nafsi ya kwanza na pili hubadilika na kuwa vya nafsi ya tatu**
**Mifano:**

1. "Tutaenda kumwona," raia walisema.
   Raia walisema kuwa wangeenda kumwona.
2. "Nitamwalika aje kwetu," baba alisema.
   Baba alisema ya kwamba angemwalika aende kwao.

d) **Nyakati hubadilika**
**Mifano:**

1. Leo huwa siku hiyo.
2. Kesho huwa siku iliyofuata.
3. Wakati ujao 'ta' hubadilika na kuwa 'nge'.
4. Sasa hubadilika na kuwa wakati huo/ule.
5. Jana hubadilika na kuwa siku iliyopita au siku iliyotangulia.

**Mifano:**

1. "Asha ataosha vyombo leo na kesho," Imo alisema.
   Imo alimjulisha Asha kuwa angeosha vyombo siku hiyo na siku iliyofuata.
2. "Niliwapa kazi ya ziada jana, kwa nini mnafanya sasa?" mwalimu aliuliza wanafunzi.
   Mwalimu alitaka kujua kwa nini wanafunzi walikuwa wanafanya kazi

ya ziada wakati huo ilhali alikuwa amewapatia siku iliyopita.

**e) 'Ki' ya masharti hubadilika na kuwa 'nge'**

**Mifano:**

1. "Ukimchapa nitakushtaki," Yaya alisema.
   Yaya alimweleza kuwa iwapo angemchapa angemshtaki.

## ZOEZI

**Ziandike sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa.**

1. "Nikipita mtihani huu nitashukuru sana," mwanafunzi alisema.
2. Sisi tunapenda kusoma, "wanfunzi walisema".
3. Kaka ataninunulia mkoba, "Poni alisema'.
4. Mjomba ametutembelea, 'Asha alieleza".
5. Nyanya alisema, "Wajukuu wangu, ninawaonya kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu."

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

1. Andika kisa kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.
2. Kuelimisha mwanamke ni kuelimisha jamii. Jadili.
3. Andika mazungumzo kuhusu amani kati ya mwalimuna afisa wa polisi.

## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

**Mbinu za lugha:**

## 1. Nahau/Misemo –

Nahau na misemo hutumika kupitisha ujumbe wa mwandishi kwa kutumia maneno ambayo hayamaanishi katika hali halisia. Misemo hutumika sana katika fasihi na katika mazungumzo ya kawaida ili kufanya lugha iwe ya kupendeza. Aidha, nahau na misemo hutumika kupunguiza makali/machukizo ya maneno katika kupitisha ujumbe uo huo.

**Mifano:**

- Kupiga moyo konde - kujituliza/kujiliwaza
- Kupiga hatua - kuendelea mbele
- Kukata kamba - kuaga dunia
- Kupiga darubini - kufanya uchunguzi
- Kutupa macho - kuangalia mbali
- Kupigwa kalamu - kufutwa kazi
- Kuandaa meza - kutayarisha chakula
- Kugonga mwamba - kutofanikiwa
- Kwenda msalani - kwenda chooni

## 2. Kejeli

Ni kutumia lugha inayoonyesha kudharau au kufanya kitu kiwe kidogo sana kuliko kilivyo. Usemi unaomuudhi mtu

## 3. Istiara

Ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kutumia kiungo 'ni' ama 'kuwa'

**Mfano:**

- mama wa kambo amekuwa mamba, nyumbani hamkaliki
- Dassa ni mkono birika, hatakupa utakacho
- masomo nayo yamekuwa mawe

## 4. Tanakali za sauti

Ni mbinu ya kutumia maneno yanayoiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika. Pia huitwa milio.

**Mfano:**

- anguka pa
- anguka mchangani tifu
- tumbukia majini chubwi
- lia kwi kwi kwi
- tiririkwa na machozi tiriri tiriri
- tulia tuli
- bingiria bingiribingiri
- nyooka twaa
- kuwa mweupe pe
- mweusi tititi

## 5. Tashbihi

Hii ni mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; 'kama', 'mithili ya', 'sawa na', 'ja'.

**Mfano:**

- mweusi kama makaa
- mweupe kama theliji
- mrembo mithili ya malaika
- baridi kama barafu
- pumbafu kama kondoo
- mwembamba kama sindano
- adimika kama maziwa ya kuku
- maridadi kama kipepeo
- mtundu kama tumbili
- pendana kama chanda na pete

## 6. Semi:

Ni fungu la maneno linapotumika kutoa maana nyingine, badala ya ile ya maneno yaliyotumika. Semi hutumika kuficha ukali wa maneno au kupamba lugha. Kuna aina mbili za semi:

a. Nahau - huwa na vitenzi
b. Misemo - haina vitenzi
c. Methali

## 7. Takriri

Ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani. Isitoshe, takriri inaweza kujitokeza kwa kurudia rudio wazo fulani katika kazi ya sanaa..

**Mfano:**

- Tumechoshwa na siasa mbaya.
- Tumechoshwa na ahadi zisizotimizwa. Tumechoshwa na miradi isiyo kamilika. Tumechoshwa na malumbano na migogoro ya kikabila. Tumechoka.

SURA YA 3

# UHUSIANO WA KIMATAIFA

**Mada Ndogo ya 1:** **Kusikiliza na kuzungumza**

**Zoezi: Kazi ya vikudi**

1. Uhusiano mzuri wa kimataifa una umuhimu gani?
2. Kwa nini ni bora mataifa tofauti yatangamane?
3. Ni njia zipi ambazo zinaweza kutumiwa kuimarisha uhusiano wa Sudan Kusini na mataifa mengine ya karibu nay a mbali?
4. Uhusiano wa kimataifa umechangia vipi kuinuka kwa chi ya Sudan Kusini?

**Mada Ndogo ya 2:** **Kusoma**

**Kifungu A**



Tukio la kihistoria lilifanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 15 Aprili, 2016 ambapo Rais John Pombe Magufuli na Rais Salva Kiir Mayardit walitia saini Mkataba wa kuiwezesha Jamhuri ya Sudan Kusini kuwa Mwanachama kamili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rais John Pombe Magufuli ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, naye Rais Salva Kiir Mayardit ni Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini.

Sudan kusini ilijiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki miezi minne baada ya nchi hiyo kupata uhuru ambapo iliwasilisha maombi yake. Baada ya miaka mitano iliweza kuwa mwanachama kamili wa Jumuiya hiyo.Jamhuri ya Sudan Kusini ilipata uhuru wake tarehe 09 Julai, 2011 na iliwasilisha maombi rasmi ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 10 Novemba, 2011. Aidha, Tangazo la kukubaliwa kuwa Mwanachama lilitangazwana Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano wa 17 wa Wakuu wa Nchi wa EAC uliofanyika jijini Arusha mwezi Machi 2016.

Rais Magufuli aliipongeza nchi ya Sudan Kusini na kusema kuwa anajivunia tukio hili la kihistoria kutokea wakati Tanzania ikiwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki .Alisisitiza kwamba ukurasa mpya wa ushirikiano na mahusiano na nchi hiyo umefunguliwa.

Kihistoria  Sudan Kusini, imekuwa  na mahusiano ya karibu na nchi za Afrika Mashariki katika nyanja mbalimbali ikiwemo mwingiliano wa tamaduni, ushirikiano wa kibiashara na uchumi na ukaribu wa kijografia. Aidha, kujiunga kwa Sudan Kusini kwenye muungano huu, kunaifanya Jumuiya hii kuwa na soko kubwa lenye takriban watu milioni 160.Dhana ya Mtangamano ni kukuza biashara, uwekezaji na miundombinu ili kujiletea maendeleo endelevu katika Jumuiya hii.

Ili Jumuiya ya Afrika Mashariki iweze kuwa na maendeleo endelevu suala la kudumisha amani ni la msingi, hivyo Sudan Kusini inapaswa kuendeleza juhudi kwenye mazungumzo ya amani.

Uamuzi wa Sudan Kusini wa kujiunga na Jumuiya ni wa dhati na una nia ya kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya wananchi wa Afrika Mashariki kwa ujumla.Sudan kusini  imeshaanza kufanyia mabadiliko mifumo mbalimbali kwenye Serikali ili kuweza kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za mtangamano ikiwemo kuunda Wizara inayoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

Wakati huohuo, Rais Kiir alitangaza kufunguliwa rasmi kwa Ubalozi wa nchi yake nchini Tanganyika na tayari alikuwa ameteua Balozi wa kuwakilisha wa Sudan Kusini nchini Tanzania.

Makubaliano yaliafikiwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itashirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Kimataifa kuhakikisha wananchi wa Sudan Kusini walioathirika na migogoro na kuikimbia nchi zingine watarejea kwa ajili ya kuendeleza nchi yao.




Chini ya masharti haya na mengine ya kimataifa, Sudan Kusini imejikakamua kimaendeleo.Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Kimataifa imeanzisha kutoa hati ya kupendeza ya kigeni. Sera ya kigeni ya Sudan Kusini inaelezewa wazi katika mandhari kubwa zaidi ikiwa ni pamoja na: Kushikamana na nchi jirani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Sudan, kuwa pamoja na nchi zingine katika kukuza umoja wa Afrika, Usawa na uwiano katika mahusiano ya kimataifa, China na Marekani.Rais wa Sudan Kusini ameunda baraza la mawaziri na amesisitizakutovumiliamaswala ya rushwa kwa umma, ubaguzi wa rangi, na upendeleo. Hii ni sera nzuri ya ndani.

Uboreshaji wa kiuchumi na kijamii ni changamoto ambazo zinakabiliwa na taifa la Sudan Kusini. Sera yetu ya kigeni inapaswa kutafakari jambo hili. Mapambano ya kijeshi hayahitajiki ila kwa matukio ya ukatili au mahitaji ya kujitetea. Kuna changamoto ya mipaka ya Jamhuri ya Sudan, hata hivyo ushirikiano wa karibu na Umoja wa Afrika na mikoa mingine ya kikanda itasaidia maendeleo ya kiuchumi na kisiasa.

Sudan Kusini inataka kuwashawishi majirani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Sudan kuwa ukuaji wa amani umejengwa kwa manufaa ya pamoja na heshima na kuwa kunahitajika ushirikiano wa kiuchumi na nchi nyingine kukuza maendeleo ya ndani.

**MASWALI**

1. Tendo la kihistoria lilitendeka wapi?
2. Toa sababu ya tendo hili kuitwa la kihistoria.
3. Ni rais wangapi waliokuwapo?
4. Taja majina ya marais hao.
5. Walikuwa marais wa nchi gani?
6. Taja tarehe za matukio yafuatayo ya Sudan Kusini :
   - i) kupata uhuru-
   - ii) kuwasilisha maombi yao ya kujiunga na jumuiya ya Afrika Mashariki
   - iii) kukubaliwa kwa ombi-
   - iv) kutia saini makubaliano-
7. Toa sababu ya Rais wa Tanganyika kujivunia tukio hili.
8. Sudan kusini imekuwa ikishirikiana na nchi zingine kwa nyanja zipi?
9. Taja mabadiliko yanayodhihirisha kukua kwa Sudan Kusini.
10. Je kulingana na kifungu, waliotoroka huko wana matumaini?

**Mada Ndogo ya 3:** **Kuandika insha**

## Vipengele muhimu katika insha

### A. Mtindo:

Mtindo ni namna insha huandikwa. Kwa mfano;
(i)Kichwa au anwani: Insha lazima iwe na kichwa au anwani na kutokana na haya ndipo mwanafunzi ataweza kuibua hoja zake.

(ii) Mtiririko wa mawazo: Inahitajika hoja zifuatilizwe kwa mpangilio, sio kwenda mbele na kurudi nyuma. Mtiririko huu wa mawazo huongozwa na sehemu zifuatazo za insha:

Utangulizi: Hii ni sehemu ya mwanzo kabisa katika insha. Inamhitaji mtahiniwa kueleza kwa ufupi mada husika. Utangulizi hujumuisha maneno

machache kama mistari mitatu au minne tu.

Mwili wa insha: Ni sehemu ambayo mtahiniwa hufululiza hoja zake katika aya mbalimbali.

Tamati: Ni hitimisho na mtahiniwa hutoa maoni, msimamo wake au hutamatisha insha yake.

## B. Maudhui

Ni hoja zinazohusiana na mada. Maudhui lazima yawe ya kutosha ili insha iweze kueleweka kikamilifu. Maudhui hayapaswi kwenda nje ya mada husika.

## C. Tahajia/ Hijai

Ni maendelezo ya maneno katika lugha. Kuzingatia mantiki katika lugha ya Kiswahili ni muhimu sana katika uandishi wa insha.

### Mfano wa makosa ya tahajia;

1. Kuunganisha maneno yanayopaswa kutenganishwa; mfano ‘nita mtembelea’ badala ya ‘nitamtembelea’, ‘Ali tuonya’ badala ya ‘alituonya’
2. Kuunganisha maneno yanayostahili kutenganishwa; mfano ‘kwavile’ badala ya ‘kwa vile’, ‘Bibiharusi’ badala ya ‘bibi harusi’

3. Kubadilisha sauti ya neno. Kwa mfano ‘shumbua’ badala ya ‘sumbua’, ‘balabala’ badala ya ‘barabara’

4. Kukata silabi mahali pasipofaa wakati neno linakosa kutoshea mwisho wa mstari. Kwa mfano: ‘Ajali ya watoto ni jambo la hatia, Serikali inapaswa kushughulikia jambo hil-i’ badala ya ‘hili’

5. Kuacha herufi katika neno mfano: ‘aliesoma’ badala ya ‘aliyesoma’, ‘Masindano’ badala ya ‘mashindano’.

6. Kuongeza herufi isiyofaa katika neno, mfano;’mutu’ badala ya ‘mtu’, ‘changua’badala ya ‘chagua’.

7. Kutoweka alama inayotarajiwa katika herufi, mfano: alama ya ritifaa ‘ngombe’badala ya ‘ng’ombe’, ‘ngangana’ badala ya ‘ng’ang’ana’. Pia

kutotumia alama za uakifishaji pale zinapohitajika au kuzitumia pale zisipohitajika. Alama hizoni kama kikomo(.), kituo(,) hisi(!) kistari kifupi(-), mabano na kadhalika.

8. Kuandika maneno kwa kifupi kwa mfano; k.m, N.k, mf.D. Sarufi
Kipengele cha sarufi ni muhimu kwa sababu sarufi mwafaka ndiyo usanifu wa lugha. Matumizi bora ya mpangilio wa maneno ya Kiswahili huwa kigezo cha kupimia matumizi ya sarufi katika insha.

## Mada Ndogo ya 4: Sarufu

Kipengele cha sarufi ni muhimu kwa sababu sarufi mwafaka ndiyo usanifu wa lugha. Matumizi bora ya mpangilio wa maneno ya Kiswahili huwa kigezo cha kupimia matumizi ya sarufi katika insha.

**Kwa mfano:**

| Analala | huyu | mtoto. | (T + V + N)- **Kosa** |
|---|---|---|---|
| ⇩ | ⇩ | ⇩ | |
| Kitenzi | kivumishi Kiashiria | Nomino | |

Mpangilio sahihi kisarufi ni, (N+V+T)- **Sahihi**

| Mtoto | huyu | analala |
|---|---|---|
| ⇩ | ⇩ | ⇩ |
| Nomino | kivumishi Kiashiria | Kitenzi |

## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

Maneno yanayofanya insha iwe na ladha. Msamiati haupaswi kuwa maneno makubwa makubwa yasiyoeleweka. Ni makosa kupachikapachika msamiati mahali popote. Msamiati unapaswa kuwa na mpangilio na uwe wa kuridhisha. Msamiati wa mtaani (sheng) au utohozi usiobadilika haupaswi kutumika kwa insha.

### AINA ZA INSHA

Kuna aina mbalimbali za insha ambazo mwanafunzi anatarajiwa kuwa na uwezo wa kuziandika. Insha hizi ni:

1. Insha za hotuba
2  Insha za kumbukumbu
3. Insha za barua
4. Insha za picha
5. Insha za mjadala
7. Insha za mazungumzo
8. Insha za mada teule

## 1. Insha ya Hotuba

Hotuba ni ujumbe unaopitishwa na yule anayetarajiwa kuupitisha. Katika hotuba, hatibu huzingatia mambo kadhaa, kama vile:

1. Hadhira itakayomsikiliza- Je, ni wazee au vijana wamejumuika pamoja?
2. Mazingira atakayotolea hotuba yake.
3. Kipimo cha hotuba yake (ili isiwendefu sana au fupi sana). Hotuba inapaswa kuwa ya wastani.
4. Hotuba ilenge mada husika bila kwenda nje ya kilichotarajiwa kuwasilishwa

## Mfano wa Insha ya Hotuba

‘Kwa Kamishna wa polisi, mkuu wa Jimbo la nile ya Juu, mkuu wa Polisi Juba Mjini, wageni waalikwa, mabibi na mabwana, wazee kwa vijana, hamjambo? Leo nimefanikiwa kuja hapa kuongea nanyi juu ya usalama wa juba mjini.

Nchi yetu ya Zawadi ni nchi ambayo inastahikiwa na wengi kwa sababu tumefaulu kuwacha tofauti zetu, na tukaamuwa kuwa na umoja na undugu unaodhihirika kila pembe ya nchi.

Juzi tu, kumetokea majangili wanaotaka kuharibu umoja na undugu wetu. Hivi majuzi kumeripotiwa visa vingi vya unyang’anyi katika maeneo tofauti tofauti humu nchini.

Swali langu ni, hawa majangili ni kina nani na wanaishi wapi? Kwa kweli hawa wahuni hawawezi kuwa wanaishi angani, la! Wamo miongoni mwetu, wengine ni ndugu na jamaa zetu. Kusema ukweli wengine wetu wanawajua hawa wahuni.

Mimi nikiwa naibu kamishna wa polisi,nashughulika na mambo ya usalama; kwa hivyo pamoja na kamishna wa polisi tumeanzisha mpango unaoitwa ‘mpango wa nyumba kumi’.Mpango huu unakuhitaji umtambue na kumfahamu unayeishi naye kama jirani yako, iwe ni kwa kijiji au ni kwa ploti.

Kila mmoja wenu ana haki kuchunguza na kujua jirani yake ni nani, anafanya kazi gani, anahusika na kina nani. Ikiwa una shauku na jirani yako basi piga ripoti kwa kituo chochote cha polisi kilichoko karibu nawe. Pia unapaswa kumfahamisha chifu wa eneo lako matukio yoyote yanayotendwa kinyume na sheria za nchi.

Kwa wakaazi wote wa mji wa Juba, ninawahakikishia kuwa usalama wa nchi umedhibitiwa kwa kila njia. Serikali imehakikisha ya kwamba kuna askari wa kushika doria usiku katika kila mtaa. Askari hawa wako tayari kupambana na uhalifu wote unaotokea saa za usiku. Ili kuunga mkono juhudi zao, amri imetolewa kuwa kila mtu anapaswa kuwa kwa makaazi yake ifikapo saa mbili

usiku. Hakuna raia atakayeruhusiwa kutangatanga njiani baada ya saa mbili usiku.
Uhalifu mwingi umekithiri katikati mwa jiji hasa vilabu vya
kuuza pombe. Amri imetolewa na serikali ya kwamba kila jumba la kustarehe linapaswa kufungwa ifikapo saa tatu usiku.

Ni matumaini yangu kuwa mtashirikiana nami na maafisa wa polisi ili tuweze kukomesha uhalifu na kudumisha usalama nchini.
Nawashukuru nyote kwa kunisikiliza. Asanteni'.

### Zoezi

1. Wewe ni kiranja mkuu wa shule. Andika hotuba utakayowahutubia wanafunzi wa darasa la nane kuhusu kujitayarisha kwa mtihani wa kitaifa.
2. Andika hotuba juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira.
3. Umealikwa uwahutubie wanafunzi wa Shule ya Mwito kuhusu umuhimu wa michezo. Andika hotuba yako.

## 2.Insha ya kumbukumbu

Insha hii anahusu taarifa ya mambo ambayo yalifanyika katika mkutano fulani. Insha ya kumbukumbu huzingatia mambo yafuatayo:

1.Kichwa cha kumbukumbu za mkutano husika. Kichwa hubeba:

a) Jina la chama au kikundi kinachokutana.
b) Mahali mkutano uliandaliwa
c) Tarehe na wakati wa kufanyika kwa mkutano huo.
d) Saa za kuanza mkutano huo.

Mfano: KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA WANACHAMA WA KIKUNDI CHA
KISWAHILI KITUKUZWE, ULIOFANYIKA KATIKA JUMBA LA SYOKIMAU TAREHE

14/05/2015 KUANZIA SAA TATU ASUBUHI

2. Sehemu ya pili hutaja mahudhurio kwa sehemu tatu:

i)Majina ya waliohudhuria mkutano. Majina haya huorodheshwa kulingana na cheo kuanzia mwenyekiti, katibu wake , mwandishi na wanachama.
ii) Majina ya waliotuma udhuru. Hawa ni wanachama ambao walikosa kuhudhuria lakini wakatuma udhuru au sababu ya kutofika mkutanoni.
iii) Majina ya waliokosa kuhudhuria mkutano na hawakutuma udhuru. Hapa majina ya wanachama ambao hawakuhudhuria na pia hawakutuma udhuru huandikwa.

3. Sehemu ya tatu ni ajenda ya mkutano. Huonyesha orodha ya mambo yatakayozungumziwa katika mkutano. Mfano;

a) Kufungua mkutano kwa maombi.
b) Mwenyekiti kukaribisha waliohudhuria.
c) Kusomwa na kuthibitishwa kwa kumbukumbu za mkutano uliotangulia.
d) Mambo yaliyotokana na kumbukumbu hizi kama vile maendelezo mabaya ya majina, maneno au kukosekana kwa jina la mwanachama ambaye alihudhuria au alituma udhuru.
e) Kufahamishwa na kuchangia kuhusu maswala yaliyowakutanisha.
f ) Maswala mengineyo.
g) Kuvunjwa kwa kikao.

**Umbo la kumbukumbu**

KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA WANAFUNZI WA CHAMA CHA USAFI WA
SHULE YA MSINGI YA KIUMINI, ULIOFANYIKA KATIKA JUMBA LA MAKTABA,
TAREHE 21/9/2015 KUANZIA SAA TATU ASUBUHI.
Waliohudhuria
1. Kimeu Mbivya - Mwenyekiti
2. Odwori Litamasi - Naibu mwenyekiti
3. Kauleni Simba - Katibu
4. Cesily Mwiko - Mwanachama
5. Lozoi Siri - Mwanachama

6. Kisau Tunda – Mwanachama

Waliotuma udhuru
1. Asonita Kisha
2. Dotai Zezeru
Wasiohudhuria bila udhuru
1. Samba Mwakale
2. Kitosha Bihale

AJENDA
1. Kufungua mkutano.
2. Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliotangulia.
3. Yanayotokana na kumbukumbu.
4. Ajenda au mada za leo
- Mikakati ya kunadhifisha mazingira.
- Ziara ya kutembelea maeneo ya pungahewa.
5. Shughuli nyinginezo.
6. Kufunga mkutano.

Kumb 1/9/15: Kufunguliwa kwa mkutano
Kumb 2/9/15: Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliotangulia.
Kumb 3/9/15: Yaliyotokana na kumbukumbu hizo.
Kumb 5/9/15: Ziara ya kuzuru.
Kumb 6/9/15: Maswala mengineyo
Kumb 7/9/15: Kufunga mkutano.

Thibitisho
Mwenyekiti _______________ Sahihi ___________ Tarehe __________
Katibu ____________________ Sahihi___________ Tarehe __________

## Zoezi

1. Andika kumbukumbu za mkutano wa Chama cha Msalaba Mwekundu uliofanyika tarehe 14/11/2015 katika shule yenu.
2. Orodhesha hatua muhimu utakayozingatia katika uandishi wa insha ya kumbukumbu.

## 3.Insha ya barua

Kuna aina mbili za insha ya barua:
i)Barua ya kirafiki
ii)Barua rasmi

Ulinganisho wa barua ya kirafiki na barua rasmi:

**Barua ya kirafiki**

1. Huwa na anwani moja.
2. Anwani ya mwandishi huandikwa upande wa kulia, pambizoni juu ya ukurasa.
3. Anayeandikiwa hutajwa kulingana na uhusiano. Mfano: Kwa Mama Mpendwa, Kwa Sahibu Wangu na kadhalika.
4. Haina mintarafu au kusudio.
5. Huanza kwa kujuliana hali au kumwamkua anayeandikiwa.
6. Lugha hutumika kulingana na mahusiano.
7. Kiwango cha urefu hutegemea anayeandikiwa na madhumuni ya kuandikiwa.
8. Mwandishi huhitimisha kwa jina lake. Sahihi si lazima iandikwe.

**Barua rasmi**

1. Huwa na anwani mbili au zaidi, ya mwandishi na ya mwandikiwa.
2. Anwani ya mwandishi inaweza kuandikwa upande wa kulia na ya mwandikiwa upande wa kushoto au anwani ya mwandishi na mwandikiwa zifululizwe upande wa kushoto.

3. Cheo cha anayeandikiwa hutajwa kirasmi; Mfano, Kwa Mwalimu Mkuu,Kwa Meneja wa Kampuni na kadhalika.

4. Mintarafu au kusudi hutajwa. Mfano MINT:KUOMBA VITABU VYA KUDURUSU

5. Haina salamu.

6. Lugha huwa ya heshima; haina utani.

7. Urefu huwa wa wastani. Malengo ya kuandika hutajwa moja kwa moja bila maneno mengi.

8. Mwandishi huhitimisha kwa sahihi kisha jina lake.

a) Barua ya kirafiki

Bhokhelo Tulia,
Shule ya Msingi ya Ndotoni,
S.L.P 00020,
Kisimani.
29/9/2015.

Kwa kaka nimpendaye,

Pokea salamu kutoka kwangu. Habari za masiku?Mimi niko mzima hapa shuleni, nalisukuma gurudumu la masomo. Kaka, mbona umenyamaza sana? Lipi la mno?

Nia ya kukuandikia barua hii ni kukukumbusha ahadi uliyonipa muhula uliopita. Unakumbuka? Najua kaka umesahau. Kumbuka wakati tulikuwa kwa nyanya uliniambia ya kwamba ungeninunulia vitabu vya Kiswahili vya kudurusu.

Bado sijasahau. Je utaninunulia lini?

Mama na baba hawajambo? Mwambie mama anitumie pesa za matumizi. Sina mengi, wasalimie kaka na dada zangu. Kwaheri.

Kakako mpendwa,

Alimosi Twindo.

**b) Barua rasmi**

Barua rasmi hulenga shughuli rasmi za kiofisi.

Mfano wa barua rasmi
DaktariZinduka Kijau,
Hospitali ya Mwangwi,
S.L.P 100,
SAILITO.
30/07/2015.

Kwa mkurugenzi,
Kampuni ya sabuni,
S.L.P 90,
SAILITO.

Kwa Bw/Bi Mkurugenzi,

KUH: NAFASI YA KIKAO JUU YA HUDUMA YA KWANZA

Ninachukua nafasi hii kukuandikia barua kuomba nafasi ya kuwa na kikao na wafanyikazi wako.

Mimi ni daktari mkuu anayesimamia hospitali ya umma ya Mwangwi katika kaunti ya Sailito. Mimi pamoja na washika dau wengine katika hospitali za

umma tungependa kuwaelimisha wafanyikazi wa sekta mbalimbali juu ya huduma ya kwanza ili waweze kuhudumia jamii kunapotokea mkasa au jambo la dharura linalohitaji huduma ya kwanza.

Kwa wakati huu, tunakusudia kutembelea kampuni zote katika wilaya ya kusini. Tayari tumeandaa vikao katika zaidi ya asilimia 75% ya kampuni hizo. Naomba utupe nafasi ili tuweze kuwa na uzinduzi huu kwa wafanya kazi katika kampuni yako kwani utawafaa sana.

Ni matumaini yangu kuwa ombi langu litakubaliwa.

Wako mwaminifu

Dzk
Dkt Zinduka kitao.

## 4. Insha ya picha

Hii ni insha inayoandikwa kutokana na picha iliyotolewa. Maelezo yanapaswa kulingana na picha hizo. Huhitaji mtahiniwa kufasiri picha vilivyo la sivyo atapotea kimaudhui.

## 5. Insha ya mjadala

Hii ni insha inayokuwa na pande mbili; kuunga mkono na kupinga. Inahitaji mtahiniwa kuwa na hoja za kutosha ili aweze kuunga mkono na kupinga. Baadaye anafaa kutoa msimamo wake anapotamatisha.

Mfano wa insha

a) Shule za mseto ni bora kuliko shule za wasichana au wavulana pekee. **Jadili**.

a. Utajiri una manufaa mengi kuliko eliMambo ya kuzingatia:
b. Uhusiano wa wanafunzi.
c. Mazingira bora ya elimu.
d. Uwajibikaji wa wanafunzi.
e. Vikwazo na vizuizi vya elimu bora.
f. Manufaa ya kila moja; shule za mseto na shule za jinsia moja.
g. Mawasiliano ya barua ni bora kuliko ya kutumia rununu. Jadili.

**Mambo ya kuzingatia:**

1. Mawasiliano haya yanachukua mkondo gani; mfano barua inaandikwa, rununu watu wanasemezana.
2. Muda unaochukuliwa na mawasiliano kwa pande zote mbili.
3. Gharama ya mawasiliano haya.
4. Faida na vikwazo vya mawasiliano haya.

### Zoezi

Andika insha ya mjadala kulingana na mada zifuatazo:

1. Kuelimisha mtoto wa kike ni bora kuliko kuelimisha mtoto wa kiume.Jadili.
2. Wanawake wanapaswa kupewa nafasi sawa za uongozi kama wanaume.

Jadili.mu. Jadili.

## 6. Insha ya mazungumzo

Insha ya mazungumzo huhusisha zaidi ya mtu mmoja. Mazungumzo haya huwa juu ya mada husika.
Mtindo wa insha ya mazungumzo ni kwamba hoja za mhusika huendelezwa baada ya hoja za mwingine. Jina la mzungumzaji huandikwa na kuwekwa nukta pacha (:) kabla ya maneno aliyoyasema kuandikwa mbele yake.

**Mfano:**
Andika insha ya mazungumzo baina ya mgojwa na daktari.

Daktari: Hujambo?
Mgojwa: Sijambo!(Anasononeka na kujishika tumbo).

Daktari: Waumwa wapi?
Mgonjwa: Nasokotwa na tumbo kila uchao.(anajishika tumbo tena kwa maumivu).

Daktari: Haya yalianza lini?
Mgonjwa: Yalianza jana usiku.

Daktari: Haya nakutuma kwa mahabara ya hapa hospitalini, uende ukapimiwe choo na mkojo kwanza kabla ya kukupa dawa(daktari anaandikaandika maandishi yasiyoeleweka kwa karatasi na kumpa mteja wake).
Mgonjwa: Asante (akiwa anasimama kuondoka).
Daktari: Kumbuka kurudisha matokeo hapa kwangu (mgonjwa anaondoka).

### Zoezi

Andika insha ya mazungumzo:
1. Baina ya mwalimu na mwanafunzi kuhusu umuhimu wa kutia bidii masomoni
.

2. Mama na mtoto wake kuhusu ugonjwa wa Ukimwi.
3. Wakili na wananchi kadhaa kuhusu hasara za mizozano ya mashamba.

## 7. Insha ya mada teule

Insha hii huhitaji mwanafunzi kutoa hoja kamili kuhusu mada husika. Ni insha ambayo huhitaji ukweli na uhakika wa mambo bila kuhangaika huku na kule au kutoa hoja zisizo za ukweli.
Mfano wa insha ya mada teule ni manufaa ya michezo ya riadha shuleni, umuhimu wa kutunza misitu, faida za wanyama pori nchini na kadhalika.

**Mfano:**

### Manufaa ya michezo ya riadha shuleni

Utangulizi: Mwanafunzi anapaswa kueleza michezo ya riadha ni ipi; kama vile mbio, kurusha mkuki, kurusha tufe, kurusha kisahani, mchezo wa jugwe, kuruka viunzi na kadhalika.

Mwili: Michezo ya riadha husaidia:

- Kujenga misuli.
- Kuwa na afya bora.
- Kuyeyusha mafuta mwilini.
- Kujenga mwingiliano/uhusiano bora kati ya wanafunzi ama wanafunzi na walimu.

- Kuondoa uchovu wa kukaa darasani.
- Huwezesha wanafunzi kutambua talanta zao mbalimbali.
- Wengine hupata nafasi ya ajira baada ya masomo.
- Kukuza maadili ya mwanafunzi kama vile uvumilivu, kukubali kushindwa, kuitikia ushindi kwa njia chanya na kadhalika.
- Mashindano mengine ya riadha hulipwa kiwango fulani cha fedha.
- Mwanafunzi anapoibuka mshindi huiletea shule yake sifa.

## Mchango zaidi kuhusu insha

Mfumo wa maswali ya insha unaweza kuwa:

1. Insha ya methali.
2. Insha ya mwanzo.
3. Insha ya tamati.

### a) Insha ya methali

Insha ya methali inahitaji mwanafunzi kutunga kisa kinachooana na maana na matumizi ya methali husika.
Ni vyema kueleza maana ya juu na ya ndani ya methali. Kisha mwanafunzi atunge kisa kinachothibitisha ukweli wa methali hiyo. Mfano:

Mtoto anaendelea na utundu wake na kupata shida inayosababishia mzazi majonzi.
Katika hatua hii mwanafunzi awe mbunifu na kuirembesha insha yake kwa tamathali mbalimbali za lugha.

Tamati: Mwanafunzi aeleze mafunzo yanayopatikana kutokana na methali hiyo.

**Zoezi**

Andika insha zinazoafikiana na methali zifuatazo:
1. Mchama ago hanyeli huenda akauya papo.
2. Zimwi likujualo halikuli likakwisha.
3. Papo kwa papo kamba hukata jiwe.
4. Cha mlevi huliwa na mgema.

## Mada Ndogo ya 6: Sarufu

**VIREJESHI ‘O’ NA ‘AMBA’**

Kirejeshi ‘O’ hutumiwa kurejelea nomino na pia kitenzi. Kirejeshi hiki hakiwezi kutumiwa pamoja na kirejeshi ‘amba’ ili kurejelea nomino iliyotajwa.

Kwa mfano:

| NGELI | UMOJA | WINGI |
|---|---|---|
| a<br>wa | Nyigu aliyeniuma ni huyu.<br>Nyigu ambaye aliniuma ni huyu. | Nyigu waliotuuma ni hawa.<br>Nyigu ambao walituuma ni hawa. |
| u<br><br>i | Mwiba uliomdunga ni mkubwa.<br>Mwiba ambao ulimdunga ni kubwa. | Miiba iliyowadunga ni mikubwa.<br>Miiba ambayo iliwadunga ni mikubwa. |
| li<br>ya | Jicho linaloona ni hili.<br>Jicho ambalo linaona ni hili. | Macho yanayoona ni haya.<br>Macho ambayo yanaona ni haya. |
| ya<br>ya | Maji yaliyomwagika ni mengi.<br>Maji ambayo yalimwagika ni mengi. | Maji yaliyomwagika ni mengi.<br>Maji ambayo yalimwagika ni mengi. |
| u<br><br>ya | Ugonjwa uliosumbua umetibiwa.<br>Ugonjwa ambao ulisumbua umetibiwa. | Magonjwa yaliyosumbua yametibiwa.<br>Magonjwa ambayo yalisumbua yametibiwa. |
| ki<br><br>vi | Kiboko kilichopotea kimepatikana.<br>Kiboko ambacho kilipotea kimepatikana. | Viboko vilivyopotea vimepatikana.<br>Viboko ambavyo vilipotea vimepatikana. |
| i<br>zi | Sahani iliyovunjika ilitupwa.<br>Sahani ambayo ilivunjika ilitupwa. | Sahani zilizovunjika zilitupwa.<br>Sahani ambazo zilivunjika zilitupwa. |
| u | Ukucha ulio mchafu umekatwa.<br>Ukucha mabao ni mchafu | Kucha zilizochafu zimekatwa.<br>Hucha ambazo ni chafu |

| | | |
|---|---|---|
| zi | umekatwa. | zimekatwa. |
| i<br>I | Sukari iliyomwagika ni nyingi.<br>Sukari ambayo imemwagika ni nyingi. | Sukari iliyomwagika ni nyingi.<br>Sukari ambayo imemwagika ni nyingi. |
| u<br>u | Usafi unaovutia unaridhisha.<br>Usafi ambao unavutia unaridhisha. | Usafi unaovutia unaridhisha.<br>Usafi ambao unavutia unaridhisha. |
| li<br>li | Giza linalotisha lipo tena.<br>Giza ambalo linaogofya si zuri. | Giza linalotisha lipo tena.<br>Giza ambalo linaogofya si zuri. |
| ki<br><br>ki | Kigodo kilichomwagika ni changu.<br>Kigodo ambacho kilimwagika kilikuwa changu. | Kigodo kilichomwagika ni chetu.<br>Kigodo ambacho kilimwagika kilikuwa chetu. |
| ku | Kuimba kulikowapendeza kumeisha.<br>Kuimba ambako kuliwapendezakumeisha. | Kuimba kulikowapendeza kumeisha.<br>Kuimba ambako kuliwapendeza kumeisha. |
| pa | Mahali palipo na maji pamezingirwa.<br>Mahali ambapo pana maji pamezingirwa. | Mahali palipo na maji pamezingirwa.<br>Mahali ambaapo pana maji pamezingirwa. |
| ku | Mahali kuliko na maji kumezingirwa.<br>Mahali ambako kuna maji kumezingirwa. | Mahali kuliko na maji kumezingirwa.<br>Mahali ambako kuna maji kumezingirwa. |
| mu | Mahali mlimo na maji mmezingirwa.<br>Mahali ambamo mna maji mmezingirwa. | Mahali mlimo na maji mmezingirwa.<br>Mahali ambamo mna maji mmezingirwa. |

## Zoezi

**Rekebisha virejeshi 'O' na 'amba' katika sentensi zifuatazo.**

1. Kiberiti kinalotumiwa ni chetu.
2. Msumari ambayo ilipigiliwa imetoka.
3. Mashati zinazofuliwa zitaanikwa.
4. Chai ziinazomwagika zimechemka.
5. Maabara linalofagiliwa yatatumiwa.
6. Bawabu ambaye linafunga mlango ni kukubwa.
7. Mkutubu inayotupatia vitabu amepotea.
8. Udhaifu linalomkumba unamlemaza.
9. Kukimbia ambacho alifanya kulimnusuru.
10. Kondeni mnapofyekwa ni kuzuri.

## Mada Ndogo ya 7: Kuandika

1. Andika insha juu ya faida za muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Maendeleo ya nchi hutegemea mahusiano yake na nchi zingine. Jadili.
3. Sudan Kusini ina nafasi nzuri za kushirikiana na nchi zingine zanazoizunguka.Thibitisha kwa maoni yako.
4. Andika kisa kuhusu umuhimu wa wananchi kushirikiana katika taifa.
5. "Amani na utangamano ni nguzo muhimu katika kurudisha ujirani mwema." Jadili.
6. Wewe ni balozi wa nch ya Sudan Kusini. Andika hotuba utakayoitoa katika kongamano la umoja wa Mataifa ukielezea umuhimu wa ushirikiano na utangamano.

SURA YA 4

# UTALII

Mada Ndogo ya 1:

## Kusoma

### Kifungu a:

### Utalii

Utalii ni hali ya kusafiri huku na huko kuyafurahia mandhari. Pia kule kushughulikia watalii au kuwahudumia ni Utalii.  WenginehuchukuliA utaliikama kitendo cha kusafiri mbali na mahali unakoishi, mfano kutoka Kenyakwenda Sudan Kusini ama pia kutoka kijijini mwako kwenda kujivinjari Juba. Kwa ufupi kuna viwango viwili vya utalii; kuna kule kutembea kutoka mahali pamoja hadi pengine katika nchi yako na kuna kutoka nchi moja hadi nyengine.

Utalii umedhaminiwa sana kwani huchangia pakubwa kuinua uchumi wa nchi. Mwanzo, vinavyovutia watalii katika nchi ni wanyama wa porini, pwani, vitu vya kihistoria, mila na utamaduni na hata mazingira.

Watalii wanaotoka nchi za kigeni huleta fedha za kigeni na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi kwani hutumiwa kununulia vitu vingine na kukuza maendeleo

nchini. Utalii pia unasaidia kuongeza idadi ya nafasi za kazi za wenyeji nchini. Watu wanavyozidi kupata kazi ndivyo uchumi unazidi kuimarika na umasikini kupungua.

Kupitia utalii, kuna utunzaji wa mazingira.  Miti huleta mvua. Kwa hivyo utunzaji wa mazingira unasaidia pakubwa kuongeza kiwango cha mvua katika sehemu mbalimbali nchini. Zaidi ya hayo, miti huwa chakula na mahali pa kuishi pa wanyama wengi.

Watalii wawekezaji ambao wengi wao huwa wakwasi, wao huwekeza katika sekta mbalimbali nchini. Wao hulipa ushuru mwingi na hivyo basi kuimarisha uchumi wa nchi.

Watalii wengi huchukua ‘picha’ za wanakotembelea na wanayoona na kisha kuwaonyesha wenzao wanaporudi nyumbani. Hii huwapa wengine hamu ya kutembelea nchi wanazoziona kwenye picha na hivyo kuongeza idadi ya watalii nchini. Idadi ya watalii inavyoongezeka ndivyo mapato kutokana na utalii yanavyozidi kuongezeka.

Sudan Kusini inaendeleza utalii japo kwa kiwango cha chini.Sekta ya utalii huchangia sehemu ndogo ya pato la Taifa la Sudan Kusini.Kulingana na ripoti ya Halmashauri ya Utalii, mchango wa kusafiri na utalii katika Pato la Taifa unatarajiwa kukua hadi kwa kiwango kikubwa kufikia mwaka wa 2024. Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Juba, ambao ndio uwanja mkubwa nchini Sudan Kusini, umepanuka kutoka kuwa wa ndege za kawaida hadi ndege za kimataifa ambazo zinafanya kazi ya usafiri.SudanKusini haina hoteli maarufu za nyota tano lakini imejikakamua na kuwa na hoteli za nyotambili tu au tatu.

Vivutio si vingi Sudan Kusini. Hata hivyo, Sudani Kusini ina mbuga 14 za kanda au maeneo ya ulinzi na uhamiaji wa wanyama. Hifadhi ya Taifa ya Boma ndio kubwa huku  vingine vikuu vikijumuishwa, Hifadhi ya Taifa ya Bandingilo, Hifadhi ya Taifa ya Lantoto, Hifadhi ya Taifa ya Nimule na Hifadhi ya Taifa ya Shambe na Hifadhi ya Taifa ya Taifa.Pia kuna hifadhi kadhaa za  ambazo zinajumuisha Ez Zeraf Game Reserve, Ashana Game Reserve, Reserve ya Bengangai, Bire Kpatuos Hifadhi ya Hifadhi, Hifadhi ya Hifadhi ya Chelkou,

Hifadhi ya Mbuga Fanikang, Hifadhi ya Mbuga ya Juba, Hifadhi ya Mbuga ya Kidepo, Hifadhi ya Visiwa vya Mbarizunga, na Hifadhi ya Nyaraka ya Numatina kati ya wengine.

Sudan Kusini pia inajulikana kwa eneo lake la mvua kubwa la Sudd, eneo la kilomita 320 na urefu wa kilomita 400. Inajulikana kama moja ya maeneo makubwa ya ardhi duniani na aina 400 za ndege zinapatikana huko.

Utalii Sudan Kusini unapatwa nachangamoto kutoka nchi za kigeni;kwa mfano Serikali ya Marekani inaonya wananchi wake dhidi ya kutembelea Sudan Kusini kutokana na migogoro ya silaha iliyoendelea nchini. Kwa ushauri uliochapishwa mnamo Desemba 2015, balozi wa Marekani Kusini mwa Sudan hawezi kutoa msaada wowote unaohitajika kwa wananchi wa Marekani au nje ya Juba kutokana na ukosefu wa miundombinu ya msingi na vitisho vya usalama . Washauri wa Canada na Uingereza pia wanapendekeza kuepuka safari zote za Sudan Kusini na maeneo ya mpaka, na pia wanaonya juu ya kutoweza kutoa msaada kwa wananchi wao Kusini mwa Sudan.Sudani Kusini ina uhamiaji mkubwawa wanyamaduniani na kwa hiyo inachukuliwa kuwa mahali pazuri pa uchumi, lakini ukosefu wa miundombinu kwa ajili ya utalii na vita vya wenyewe kwa wenyewe vinaendelea kuchukuliwa kama changamoto kwa sekta ya utalii.

## MASWALI

1. Utalii ni nini?
2. Taja viwango viwili vya utalii kulingana na kifungu.
3. Watalii wengi huvutiwana nini?
4. Eleza umuhimu wa miti kulingana na kifungu.
5. Kulingana na kifungu watalii matajiri wana faida gani?
6. Kuna faida gani ya watalii kuchukua picha wanapozuru nchini?
7. Eleza faida ya kuongezeka kwa watalii katika maeneo fulani.
8. Kwa mujibu wataarifa, Sekta ya utalii iko vipi Sudan Kusini?
9. Taja mabadiliko katika uchukuziwa ndege wa Sudan Kusini.
10. Taja hifadhi za wanyama zilizoko Sudan Kusini.
11. Eneo la ndege wa kuvutia ni lipi?
12. Eneo hili liko na idadi ipi ya ndege?
13. Taja mataifa yanayorudisha nyuma utalii wa sudan kusini.

14. Mataifa haya yanatoa sababu gani ya hatua hii?
15. Ni nini kinazuia utalii kupata mizizi Sudan kusini kulinganana aya ya mwisho?

**Kifungu b:**

Utalii tanzania

Utalii ni moja kati ya sekta zinazoingiza kipato kikubwa kwa taifa la Tanzania kwa kipindi kikubwa. Nchi hii imejaliwa rasilmali halisia nyingi ikiwemo mito mikubwa na midogo, mabonde na milima yenye viumbe vya kuvutia na kushangaza kamambega,vyula,kima,nyani,tumbili,vinyonga,viboko,mamba.Pia ina mbuga za wanyama sio chini ya saba kubwa kama;Katavi, Mikumi, Ngorongoro, Serengeti, Manyara, Tarangire, Selou, Ruhaa, Mkomanzi, Kitulo na nyinginezo ndogondogo.



Tanzania inavivutio vingi ambayo mataifa mengi Afrika na kwingineko duniani hawana kama maporoko ya Kalambo, Ndola waterfalls na Irente view. Hata hivyo, mapato ya nchi hii yanayotokana na utalii ni duni sana yakilinganishwa na nchi jirani ya Kenya.Kuna mambo kadhaa ambayo yameifanya sekta ya utalii

Tanzania isilete fedha nyingi zaidi na hivyo kutochangia zaidi kwenye pato la taifa.

Jambo la kwanza ni matangazo. Hii ina maana kwamba vivutio vya utalii vya Tanzania havitangazwi; yaani ukilinganisha na Kenya, unagundua kuwa Kenya wanatangaza vya kwao mara 12 zaidi kuliko Tanzania.

Tafiti mbalimbali za nchi zilizofanikiwa kiutalii duniani zinaonyesha kuwa vivutio vya utalii vinavyotangazwa zaidi ndivyo huleta watalii wengi zaidi na hivyo kuingiza fedha nyingi zaidi. Nchi ya Tanzania ina ukosefu wa mabandiko na matangazo yanayoonyesha vivutio kwenye miji na maelekezo yanayoonyesha vivutio vingine vilivyopo kwenye miji ya jirani. Hii inaathiri sana ubora wa kuwajuvya watalii juu ya vivutio nchini.Jambo jingine ni kuwa mabasi ya abiria toka Dar es Salaam kwenda mikoani na nchi jirani hayana vipindivya kutangaza utalii, hata yale yanayovuka mipaka kwendanchi jirani yanashughulika na filamu za kigeni kama Kichina, Kihindi hata filamu zinazoonyesha utalii.Wao pia wangeweza kutangaza utajiri wa nchi hii kwa kuweka filamu zinazoonyesha milima,mabonde,mito,mbuga na kila kilichopo na maelekezo yake kwa lugha ya msafiri kama vile Kiingereza, Kifaransa,Kijerumani, Kichina na kadhalika.

Jambo jingine ambalo limekuwa likilalamikiwa na wataalamu wa uchumi na wadau wa sekta ya utalii kwa muda mrefu ni mazingira yasiyo rafiki na utalii au vivutio, ni kuanzia kwenye suala la usafiri.Watalii wanalalamikia kukosekana kwausafiri wa ndege nchini Tanzania. Kenya wana Shirika lao la Ndege na hivi sasa linafanya kazi kwenye nchi nyingi zinazotoa watalii, kwa hivyo watalii wana uhakika wa kupanda “Kenya Airways” za Kenya kutoka ughaibuni hadi Tanzania.

Tanzania haina huduma za kirafiki za usafiri wa uhakika ambao unaweza kuwafanya watalii wafurahie na wapate maelekezo mbalimbali juu ya vivutio vya nchi hii. Kwa sehemu kubwa watalii wanaotembeleaTanzania wanahudumiwa na magari ya kukodisha yaliyosajiliwa na usajili wa nchi za nje kama Kenya au Afrika Kusini yakiwapeleka kutembelea vivutio nchini humo.Kuna uchache wa huduma ya usafiri wa anga kutoka mahali pamoja hadi pengine, wakati wote wa siku, hali inayoonekana kuathiri utalii.

Huduma za maji safi maeneo yote yaliyopo karibu na vivutio hivi hazijaboreshwa kufikia viwango vya kimataifa.Pia huduma bora za afya na usafi yakinifu maeneo yote husika ya vivutio vya kitalii hayavutii.Kuna ukosefu wa uboreshaji wa miji inayozunguka maeneo haya,yakikosa hoteli au vyumba vya kulala vya kisasa vya kitalii.

Ukosefu wa maeneo muhimu ya wao kupata mahitaji yao ya manunuzi ya vifaa na vyakula maalumu kama Shop malls, kuwepo kwa masoko ya kisasa yenye vitu vilivyo hifadhiwa vizuri unakatiza tamaa ya utalii.Maeneo mengi ya chakula na huduma nyingine kama mahali pa mapumziko, michezo kwenye miji hiyo yanayolingana na maisha yao hayapo.Kwa upande wa vyakula vyao na tamaduni zao tofauti kama vile vya Kiulaya, Kiamerika, Kitaliano, Kirusi na za Kiafrika na Kitanzania havimo. Kwa sasa kila mahali utakuta ugali, wali nanyama tu. Nchi ya Tanzania inahitajika kuwa na chakula cha kienyeji kinachowaovutia watalii ilikuepushe tabia ya wao kuja na vyakula na vitu vingine toka wanakotoka.Ni vizuri kuwajengea tabia ya kununua vitukama vyakula na matunda kwa wingi kwenye miji waliofikia.

Kwa kila njia na nia serikali ya Tanzania inaweza kutatua changamoto hizi kwa njia mbalimbali. Kwanza iongeze bajeti ya kutangaza utalii kwa kiasi kikubwa sana ili kupambana na kuwashinda Kenya. Na pili ni ijenge mazingira rafiki kwa ajili ya watalii kuwa na usafiri rahisi wa kutoka kwenye nchi muhimu za nje kuja Tanzania moja kwa moja na kuboresha mazingira ya vivutio vya utalii ili yawe rafiki sana kwao.

Serikali iwekeze kwenye miundombinu barabara za uhakika na usalama wa kutosha. Usafiri wa anga uendelee kuimarishwa hasa kwenye maeneo yenye vivutio hivi.

Miji Mikubwa kama Mwanza,Dar,Arusha,Mbeya na mingine inayokuwa pamoja na Zanzibar iwekwe mabango maalumu kwa wageni kupata habari za vivutio iwe kwa magari watakayotumia ikipeperushwa kwa lugha yao.

Tamaduni zibadilishwe na ziwe ya kutangaza vivutio toka mashuleni hadi kazini, kama kuna wageni wapewe safari maalum za kipekee kwenda kwenye vivutio ili wawe mabolozi wa vivutio hivi nchini mwao.

Utalii hauishii mbugani, miji inapaswakuandaliwa, usafiri uwe maalumu kwa watalii, tamaduni na vyakula vyao viandaliwekikwetu, mazingira yawe na usalama wa kutosha na vitumbuizi vinavyoashiria kuja kwao kunafurahiwa.

Ni jambo la busara kuwajengea utamaduni watu wa mataifa ya nje kufanya likizo zao Tanzania na watoke kwao moja kwa moja kuja Tanzania bila kutua nchi nyingine za jirani au za mbali kama Afrika kusini na kwenda Tanzania kama mahali pa kumalizia ziara zao.Watalaam waliobobea kwenye mambo ya kiutalii na uchumi wahusishwe katika kuandaa maandiko yanayoweza kuchora mpango wa uboreshaji wa sekta ya utalii.Utalii ni muhimili wa uchumi wa nchi yoyote ile inayonuia kukua, ilindwe.

**MASWALI**

1. Taja manufaa ya sekta ya utalii katika nchi ya Tanzania kulingana na aya ya kwanza.
2. Taja aina mbili za rasilmali zilizo nchini Tanzania.
3. Taja wanyama wanaopatikana Tanzania.
4. Orodhesha hifadhi za wanyama nchini Tanzania.
5. Ni nini ambacho nchi zingine zinakikosa lakini kiko Tanzania?
6. Taja vituo vitatu vya Tanzania.
7. Mapato ya utalii ya Tanzania yakoje?
8. Matangazo ya utalii Tanzania yako na shida zipi?
9. Nchi inayolinganishwa na Tanzania kamatangazo ya utaliini ipi na imewashindaje?
10. Utafiti unaonyesha nini juu ya kutangaza utalii?
11. Ukosefu wa mabango ya matangazo ya usafiri una athari yoyote?
12. Usafiri wa mabasi unalaumiwa vipi?
13. Mabasi yanapewa ushauri gani?
14. Eleza malalamishi kwa upande wa usafiri wa ndege.
15. Usafiri wa magari ya kwenda vivutioni una shida gani?
16. Je usafiri wa anga kwenda vivutioni unaridhisha? Toa sababu.
17. Taja vitu vingine vitatu ambavyo havivutii.
18. Mwandishi analalamikia nini juu ya chakula katika maeneo ya vivutio?
19. Je nchi ya Tanzania inaweza kubali hali yake ya utalii? Thibitisha kwa hoja tatu.

20. Mwandishi anamaanisha nini anaposema “Utalii ni muhimili wa uchumi wa nchi”?

## Mada Ndogo ya 2: Sarufi

**UUNDAJI WA NOMINO**

a) Kutokana na vitenzi vya kigeni

Hivi ni vitenzi ambavyo asili yake si kibantu.Vitenzi vya asili ya kibantu huishia kwa irabu ‘a’ kama havijanyambuliwa. Vitenzi vyenye asili ya kigeni huishia kwa irabu i, u na e.

Mifano ya vitenzi vyenye asili ya kigeni:

a) jadili
b) sali
c) samehe
d) hukumu
e) hubiri
f) dhamini

**Uundaji wa nomino**

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| a) jadili<br>b) sali<br>c) samehe<br>d) shiriki<br>e) safiri | mjadala<br>sala<br>msamaha<br>shirika/mshirika<br>safari/msafara/msafiri |

**Zoezi**

**Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.**

1. zuru
2. fariji
3. kashifu
4. uza
5. hubiri
6. dharau
7. dhuru
8. abudu
9. hukumu
10. ahidi

## Mada Ndogo ya 3: Kuandika

1. Eleza umuhimu wa utalii.
2. Taja vivutio vya utalii katika nchi yako.
3. Jadili changamoto zinazoikumba sekta ya utalii katika nchi yako.
4. Andika kisa kuhusu safari yako kwenye mbuga ya wanyama.
5. “Utalii ni mojawapo ya vitega-uchumi katika nchi ya Sudan Kusini.” Jadili.
6. Andika mazungumzo baina ya mwelekezi wa mbuga ya wanyama na mtalii.

SURA YA 5

# TAMADUNI, URITHI NA UTAMBULISHO

**Mada Ndogo ya 1:** **Kusikiliza na kuzungumza**

1. Utamaduni ni nini?
2. Nani anayebuni tamaduni za jamii?
3. Utamaduni una umuhimu gani katika jamii?
4. Kwa nini ni vyema kuzitunza na kujivunia tamaduni zetu?

**Mada Ndogo ya 2:** **Kusoma**

Watu wengi hupenda kufikiria utamaduni ni vitu ambavyo tunavyoviona kama mapishi, mavazi, ngoma, muziki, kama desturi ya sherehe.Utamaduni ni jinsi

binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake.Pia imeelezwa kuwa, neno "utamaduni" linatumika kimsingi katika njia tatu zifuatazo: - kwanza kama maonjo ya hali ya juu katika sanaa, vile vile hujulikana kama utamaduni wa juu,na tatu kama mkusanyiko wa maarifa ya binadamu.

Utamaduni ni shughuli au kazi zote afanyazo mwanadamu na namna anavyokabiliana na mazingira yanayomzunguka ili kukidhi mahitaji yake muhimu ya kumwezesha kuishi. Mahitaji hayo muhimu ni chakula, makazi na mavazi. Katika kumwezesha kupata mafanikio aliyotarajia katika kupata mahitaji hayo, binadamu alijiwekea utaratibu (nguzo) za msingi katika kutekeleza shughuli zake za kila siku.

Wahenga walinena ***mkataa kwao mtumwa.***Usemi huu unatufundisha mambo mengi sana ukizingatia mwenendo wa maisha katika mazingira ya sasa. Kifupi, usemi huu una maana kwamba, mtu ambaye anadharau maisha na tamaduni ambazo amekulia nazo, ametekwa kimawazo na yuko tayari kutumikishwa au kufuata mila na desturi za jamii nyingine kutokana tu na tofauti ya tamaduni hizo.

Lugha hunasa muhimu wa desturi ya jamii fulani. Kutokana na lugha, unafahamu dhana yake ya msingi juu ya mtu binafsi jinsi wanavyohusiana kwa vikundi, matarajio ya jamii, sherehe za jadi na maadhimisho na majukumu ya jamii kwa mtu binafsi.

Matatizo hutokea wakati tamaduni mbili au watu wawili kutoka tamaduni tofauti, hasa, hujaribu kuingiliana na kila mmoja katika uhusiano. Matatizo hayo yanayotokana na mgongano miongoni mwa matarajio yalio chini ya nafsi iliyofichika na iliyo wazi kutoka jadi. Ili kuitikia mambo ya nje, kila kundi la jamii linajaribu lakini kila kundi linahusiana tofauti na lingine. Kila kundi la utamaduni linadhani njia yao ni sahihi, ni "maarifa ya kawaida" tu ambayo inapaswa kila mtu ajue. Matatizo hayo yanaitwa "utamaduni mshtuko" haswa wakati mtu mmoja anapojaribu kukaa miongoni mwa watu wa jamii tofauti.Walakini, hakuna utamaduni wa jamii fulani ambao hauna maarifa na ujuzi kutatua kwa urahisi matatizo kutokana na utamaduni mshtuko. Kwa hivyo, migonganomidogo au mikubwa inatolewa.

Kushindwa kutatua migogoro hii husababisha madhara katika ngazi mbalimbali, kama vile; katika ngazi za kikabila ambapo mgogoro utakuwa vita. Katika ngazi ya mtu binafsi migogoro husababisha ubaguzi wa rangi na kunyanyasa wengine. Katika ngazi ya kati ya kimapenzi mahusiano, migogoro husababisha talaka na huzuni.

Utamaduni hufungwa na miko katika makabila tofautitofauti.Watu wengi kwa kutokujua maana na dhamira ya kuweka miko na makatazo katika mila na tamaduni zetu, wamekuwa wakiona kuwa miko na baadhi ya makatazo huwa imepitwa na wakati au haikupaswa kuwepo.Hii inaweza kuwa ni kweli kutokana na maendeleo tuliyo nayo hivi sasa lakini mila na makatazo hayo yalikuwa ni kwa faida kwa walengwa kwa wakati ule na miiko ilisaidia sana katika kudumisha usafi, usalama na kuheshimiana katika jamii.

Wakale ambao ni mababu zetuwaliweka miiko kwenye jamii husika kwa sababu kadhaa.Wakale waliamini miiko inazuia makosa kadhaa katika jamii.Pia kwamba kukiuka miiko kuliweza kuleta athari fulani katika jamii.
Baadhi ya mila na tamaduni mbalimbali zinachuliwa kama aidha hazikutakiwa kuwepo katika jamii au zilikuwa na lengo la kunyanyasa au kumnyanyasa mwanamke au hata kumshushia hadhi yake.

Wengi wetu tunajiuliza maswali juu ya baadhi ya miiko ambayo wengi wetu tumekutana nayo kwenye jamii mbalimbali au makabila mbalimbali ni kama hii ifuatayo: mfano, kupiga mluzi usiku, unamwita shetani. Hii ni kati ya imani ambazo zilianza kipindi kile ambacho machifu ambao walikuwa wakishirikiana na walowezi (Wazungu) kukamata watumwa.

Upigaji wa miluzi ilikuwa ni njia mojawapo ya kuwataarifu watu kuwa kuna hatari kwa hali hiyo wajihadhari.Sababu nyingine ni kuwa kipindi cha usiku kuna baadhi ya wadudu hatari kama vile nyoka, ambao wanavutiwa na sauti za miluzi. Kwa hivyo unapaswa kuelewa kuwa miiko na makatazo mengi yalikuwa au yaliwekwa kwa namna ya kumtisha mfanyaji au mkusudiwa ili ajenge woga

na kuacha kufanya jambo fulani. Hata hivyo, jambo la msingi hivi sasa ni kuhakikisha kwamba elimu zaidi inatolewa juu ya athari inayotokana na baadhi ya miko, mila na desturi potofu na kuendeleza zile ambazo bado ni msingi imara katika kuendeleza utamaduni wetu.

Ni wazi kwamba, maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano na kuongezeka kwa utandawazi kumechochea zaidi mabadiliko yaliyopo katika jamii katika nyanja ya utamaduni. Tofauti zilizopo katika suala zima la kufuata mila na desturi zinatokana na vijana wengi kujifunza kutoka nchi za kigeni.Aidha, matumizi ya mavazi yasiyo na heshima yamechangia mambo mbalimbali kwa mfano kuhamasisha vitendo viovu na vya kihuni kama vile ukahaba na ubakaji.

Matumizi ya vyakula vya asili yana faida mbalimbali kwa binadamu katika kujingika na maradhi mbalimbali, kujenga na kuimarisha virutubisho vya mwili. Matumizi ya vyakula vilivyokaa kwenye majokofu kwa kipindi karibu wiki moja au zaidi vinapoteza ladha yake ya asili na pia hata virutubisho vyenyewe vinapungua au kupoteza kabisa nguvu yake. Aidha vipo vyakula vilivyozalishwa katika mazingira yasiyo ya asili mfano kuku wa kisasa. Vyakula hivi vimekuwa vyanzo vikubwa vya matatizo ya kiafya miongoni mwa watu.Wakati umefika kwa jamii zetu kutambua, kuenzi na kuendeleza tamaduni zetu ambazo tumezirithi kutoka kwa mababu na bibi zetu ili kizazi kipya nacho kiweze kufaidika na tamaduni hizo.

**MASWALI**

1. Watu wengi hupenda kufikiria utamaduni nini juu ya utamaduni?
2. Toa maana ya utamaduni kulingana na aya ya kwanza.
3. Taja njia tatu zinazotumiwa kuelezea utamaduni.
4. Eleza utamaduni kama njia ya kukudhi mahitaji ya mtu.
5. Eleza maana ya methali ‘mkataa kwao ni mtumwa’.
6. Lugha husaidiaje katika utamaduni?
7. Utamaduni mshtuko ni nini?
8. Ainisha ngazi ambazo huathiriwa watu wanaposhikilia kuwa utamaduni wao ni bora kuliko wa wengine.
9. Taja aina tatu za migogoro ambayo hutokea watu wanaposhikilia kuwa utamaduni wao ni bora kuliko wa wengine.

10. Je, ni kila mtu huona miiko kwa njia chanya?
11. Toa sababu maelezo mawili ya mwiko wa kutopiga mluzi usiku.
12. Ni nini kimeathiri mila na utamaduni wetu kulingana na kifungu?
13. Taja athari ya mavazi yasiyofaa.
14. Je, vyakula vya kiasili vinafaida yoyote?
15. Mwandishi anahimiza nini katika aya ya mwisho?

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

## Sentensi za kiswahili

Sentensi ni neno ua kundi la maneno yenye kiima na kiarifa.

## Aina za Sentensi

### a) Sentensi sahili

Hii ni sentensi yenye kishazi kimoja na huwakilisha wazo moja tu. Inaweza undwa kutokana na kikundi tenzi pekee au kikundi nomino pamoja na kikundi tenzi.

Mifano:

1. Wanasoma.
2. Ataimba.
3. Deng anakimbia.
4. Mari anafagia.
5. Mkulima anvuna mahindi.

### b) Sentensi ambatano

Hii ni sentensi yenye Zaidi ya kishazi huru kimoja. Huwakilisha mawazo mawili au Zaidi. Mara nyingi, sentensi hizi huundwa kwa kuunganisha sentensi mbili. Hivyo basi kuna matumizi ya viunganishi au alama za uakifishaji kama vile koma, na nusu-koloni ili kubainisha wazo moja toka nyingine.

Mifano:

1. Mama amefua nguo na kuzianika.

2. Mwalimu alitupa zoezi kisha akalisahihisha.
3. Mkulima ameyavuna mahindi na kuyauza.

**c) Sentensi changamano**

Hii ni sentensi inayoundwa kwa kuunganisha kishazi huru pamoja na kishazi tegemezi au sentenzi mbili kwa kutumi o-rejeshi ili kuleta Zaidi yawazo moja.
Mifano:

1. Deng alinileteа kalamu ambayo nilikuwa nimeitafuta kwa muda nrefu.
2. Yeye ndiye mwanafunzi hodari aliyetuzwa jana.

**Zoezi**

Kwa kurejelea maelezo hapo juu, kwa kila aina ya sentensi, tunga sentensi tano.

**Mada Ndogo ya 4:** **Kuandika**

1. Andika kisa kuhusu utamaduni uliopitwa na wakati.
2. Andika insha kuhusu umuhimu wa utamaduni.
3. Si kila mila ni potovu.Jadili.
4. Eleza jinsi mila zingine zinawakandamiza wanawake katika jamii yako.
5. Jadili jinsi watu wanaweza kuhifadhi utamaduni wao.

SURA YA 6

# HAKI ZA MWANANCHI

Mada Ndogo ya 1:

## kusikiliza na kuzungumza

**Zoezi 1: Kazi ya vikundi**

1. Taja haki zako.
2. Umewahi kudhulumiwa haki zako? Vipi?
3. Umewahi kuzidhulumu haki za mwenzako? Vipi?
4. Utarekebisha vipi tabia za kuwadhulumu wengine haki?

**Zoezi 2: Kazi ya vikundi**

1. Kwa nini haki za binadamuni muhimu?
2. Ni nani ana wajibu wa kuhakisha kuwa haki za raia hazidhulimiwi?
3. Wazazi wana wajibu gani kwa watoto wao?
4. Simulia kisa kuhusu haki zako.

5. Soma sentensi zifuatazo kuhusu haki za watoto.






Watoto wana haki ya maoni yao kuzingatiwa ... nao wana wajibu wa kuzingatia maoni ya wengine.







Watoto wana haki ya kupoke matibabu bora ... nao wana wajibu wa kujitunza vilivyo.






Watoto wana haki ya kuppata elimu bora ... nao wana wajibu wa kusoma kwa bidi na kuwaheshimu walimu wao.





Watoto wana haki ya kupendwa na mahitaji yao kutimizwa ... nao wana wajibu wa kuwapenda na kuwajali wengine.



Watoto wana haki ya kupokea huduma maalum kulingana na mahitaji yao ... nao wana wajibu wa kuishi maisha ya kujitosheleza.



Watoto wana haki ya kujivunia tamaduni na imani zoa za kiasili ... nao wana wajibu wa kuziheshimu tamaduni na imani za wengine.






Watoto wana haki ya kuishi katika mazingira matulivu na safi ... nao wana wajibu wa kushiriki katika kuchangia mazingira safi.



Watoto wana haki ya kukosea ... nao wana wajibu wa kujifunza kutokana na makosa yao.





Watoto wana haki ya kupata lishe bora na ya kutosha… nao wana wajibu wa kuhakkisha kuwa hawatupi chakula.

Zoezi

1. Orodhesha haki za watoto.
2. Orodhesha wajibu wa watoto.
3. Tunga sentensi ukitumia msamiati wa haki za watoto.

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

Soma kifungu kifuatacho.

### Haki za binadamu

Haki za binadamu ni wazo la kuwa kila mtu anastahili haki kadhaa si kwa kutegemea cheo, taifa, tabaka, jinsia, dini kwa sababu tu yeye amezaliwa binadamu. Haki hizi zimeorodheshwa hasa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu lililotolewa na Umoja wa Mataifa mwaka 1948. Tamko hilo ni kamilisho la majadiliano kuhusu haki hizo yanayoendelea. Hoja ya msingi ni kwamba, "Watu wote wamezaliwa huru; hadhi na haki zao ni sawa. Wote wamejaliwa akili na dhamiri, hivyo yawapasa watendeane kidugu.

Haki maana yake ni stahili ambazo mtu anazo kama kiumbe hai. Ni vitu muhimu ambavyo anapaswa kuwa navyo ili afaidi utu wake kama binadamu.

**Aina za haki**

Haki za Binadamu zimegawanywa katika makundi matatu: - Haki za kizazi cha kwanza, Haki za kizazi cha pili na Haki za kizazi cha tatu.

**Haki za kizazi cha kwanza**

Hizi ni haki za Binadamu ambazo ni za kiraia na kisiasa zinaonekana kuwa ndizo haki za msingi zilizozaa falsafa yote ya haki za binadamu. Kwa namna zilivyo zinaitaka dola ijizuie kufanya aina yoyote ya vitendo dhidi ya mtu binafsi ili mtu huyo aweze kuwa huru katika kujitafutia furaha na ustawi kwa kiwango kinachokubalika. Kwa kawaida, dola huchukua hatua chanya vilevile ili kuhakikisha kuwa watu wanapata haki zao za kisiasa na za kiraia. Haki za kiraia zinajumuisha “haki za hadhi ya kimaumbile” kama vile haki ya kuishi, uhuru wa kutoteswa na “haki” za michakato mingine kama vile uendeshaji wa kesi kwa

haki, kumchukulia mtu kuwa hana kosa, mambo ambayo hayawezi kupatikana kwa dola kujizuia kufanya mambo mengine tu.

Kimsingi, haki za kisiasa ni uhuru wa mawazo, dhamira, imani, kujieleza, kuchanganyika na mkusanyiko. Zinajumuisha vilevile haki ya kushiriki katika utawala wa nchi pamoja na kushiriki na kupiga kura katika chaguzi zilizo huru. Kwa mfano:-

- Haki ya kuishi,
- Uhuru, usalama, usawa mbele ya sheria,
- Usawa wa Binadamu,
- Haki ya faragha,
- Haki ya kuabudu/kutoabudu dini/imani,
- Haki ya kutoa maoni,
- Haki ya kujiunga na chama/shirika,
- Haki yakukusanyika,
- Haki ya kushirki katika masuala ya umma,
- Haki ya kushiriki mambo ya kisiasa.

**Haki za kizazi cha pili**

Hizi ni haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Haki hizi hujulikana kama haki chanya ambazo hapo awali baadhi ya watu waliziona kuwa ni za "matamanio" Kwa mfano: Haki ya kufanya kazi katika mazingira mazuri, Haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi, Haki ya kiwango cha kujitosheleza kwa chakula, Haki ya afya, Haki ya kupumzika, burudani, na starehe, Haki ya kupata elimu, Haki ya kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya jamii yake.

**Haki za kizazi cha tatu**

Kizazi cha tatu" ni kizazi kipya na baadhi ya wakati huitwa haki za "makundi" au za "mshikamano". Haki hizo ni kama vile haki ya kuwa na amani, mazingira yaliyo salama na haki ya kupata maendeleo. Katika haki za aina hii, ndimo zilimo haki za makundi maalumu kama vile wanawake, watoto na makabila ya watu wachache hasa makundi ya wenyeji asilia na watu wenye ulemavu ambao kihistoria walikuwa wametengwa. Kuchipuka kwa mtindo wa kuingizwa katika mfumo wa utaratibu wa nchi na kutambulika kwa haki hizi kunaonyesha jinsi ilivyo muhimu kwa jumuiya ya kimataifa kutambua kuwa haki za Binadamu.

Haki hizi ni kama zifuatazo:- Haki ya maendeleo, Haki ya mazingira safi na usalama, Haki ya Amani ya dunia, Haki ya kutumia rasilimali za nchi na Haki ya kujitawala.

## ZOEZI: JADILI

**Haki za mtu aishiye na virusi vya ukimwi**

Kimsingi mtu aishiye na virusi vya ukimwi ana haki zote za binadamu za vizazi vyote na kama zilivyoanishwa katika Katiba. Kwa mfano mtu aishiye na virusi vya ukimwi ana haki zifuatazo;

- Haki ya kutobaguliwa na sheria, mtu au chombo chochote katika kutekeleza majukumu yake.
- Haki ya faragha.
- Haki ya kutolazimishwa kupima afya.
- Haki ya kujieleza, kutoa maoni.
- Haki ya kupata habari.
- Haki ya kuoa au kuwa na familia.
- Haki ya kutembea ndani na nje ya Jamhuri ya Sudan Kusini.
- Haki ya kufanya kazi.
- Haki ya usawa.
- Haki ya kuthaminiwa utu wake.
- Haki ya kuishi.
- Haki ya ulinzi na hifadhi.
- Haki ya kupata matibabu.
- Haki ya kutunzwa, kuangaliwa.
- Haki ya kupata ushauri juu ya afya.
- Haki ya chakula.

Je, unaweza kuchangia vipi kuhakikisha kuwa haki zilizotajwa hapo juu na zinginezo zinatimizwa katika jamii?

# Sarufi

## Kundi Nomino na Kundi Tenzi

Kama tulivytaja hapo awali, kuna aina tatu za sentnsi.

a) Sentensi sahili
b) Sentensi ambatano
c) Sentensi changamano

Tunapochanganua sentensi, tunazingatia kundi nomino na kundi tenzi. Kundi nomino huelekeza kwa mtenda, mtendwa na mtendewa.

Kundi nomino huundwa na:

a) nomino moja au mbili zilizounganishwa
b) nomino na kivumishi
c) kiwakilishis
d) viwakilishi na vivumishi
e) kitenzi jina
f) kitenzi jina na kivumishi

Mifano:

1. *Mtoto* anakula chakula.
2. *Jirani yangu*ni mkali.
3. *Sisi* tunapenda michezo.
4. *Nyinyi wenyewe* mliwaona.
5. *Kuimba*ni kuzuri.
6. *Kucheka kwake* kunaudhi.

**Kundi Tenzi**

Hii ni sehemu ya sentensi inayoeleza kitendo kilichofanya, kifanywacho au kitakachofanya. Sehemu hii ya sentensi inaweza kujisimamia kwa kuwa na viambishi viwakilishi vya kundi nomino. Kundi tenzi huundwa na:

1. kitenzi kikuu

2. kitenzi kishirikishi au kitenzi kisaidizi na vitenzi vikuu
3. kitenzi na shamirisho
4. kitenzi na chagizo

Mifano:

1. Mwanafunzi *anasoma*.
2. Mwanafunzi *amekuwa akisoma*.
3. Baba *amenunua baiskeli*.
4. Nyanya *anatembea polepole sana*.

**Zoezi**

**Onyesha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi zifuatazo.**

1. Kuimba kwake kumewavutia wengi.
2. Sisi wenyewe tuliamua kwenda kazi.
3. Deng na Mari ndio waliokosakufika darasani.
4. Mvuvi amevua samaki wengi wakubwa.
5. Vile vyao viliharibiwa na mafuriko ya maji.
6. Nahodha anaendesha meli.
7. Amehuzunika.
8. Mwanamke huyu husuka nywelw.
9. Mti umeanguka.
10. Kitabu kilichokuwa kimepotea kimepatikana.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

1. "Kumwajiri mtoto ni kumdhulumu." Jadili.
2. Andika insha inayoishia kwa maneo yafuatayo.
   … Mwinyi Hatibu alikijutia kitendo chake cha kuwaajiri watoto katika shamba lake la mpunga.